**26 JUNI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

______

## MAJADILIANO YA BUNGE

______

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Hamsini na Nane – Tarehe 26 Juni, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge na tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mbunge wa Itigi, sasa aulize swali lake.

Na. 687

### Kukamilisha Maboma ya Zahanati – Itigi

**MHE. YOHANA S. MSITA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa maboma ya zahanati katika Jimbo la Itigi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, Mbunge wa Jimbo la Itigi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Takwimu zilizokusanywa hadi kufikia mwezi Mei, 2026 zimeainisha jumla ya maboma 1,841 ya zahanati kote nchini ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Itigi ina jumla ya maboma matano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ilitoa shilingi bilioni 17.36 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 346 ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Itigi ilipokea jumla ya shilingi milioni 150 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati tatu za Njirii, Mlongojii na Kintanula.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi yakiwemo maboma matano katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, swali la nyongeza.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri

kuhusiana na mambo ya zahanati katika Jimbo la Itigi. Sasa nina ushauri, lakini nina swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kata za Ipande kwa maana ya Vijiji vya Mkajenga, Kata ya Mwamagembe katika Kitongoji cha Matumaini, lakini Kata ya Gondi, Damwelu pamoja na Idodyandole hazina vituo vya afya na huduma ziko mbali na maeneo haya yana maboma tayari.

Sasa ninaomba katika vipaumbele ambavyo Serikali itatuletea fedha, maeneo haya yapewe kipaumbele cha kwanza ili yaweze kujengewa maboma pamoja na jengo la *RCH* pale Itagata, pamoja na nyumba ya watumishi pale katika Kijiji cha Mgamboo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la nyongeza la pili, ni kwamba nini mpango wa Serikali sasa katika kuongeza vifaa katika zahanati nyingi ambazo zimekuwa kwa kweli zina upungufu wa vifaaatiba katika Jimbo la Itigi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo ameuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kusisitiza maeneo yenye vipaumbele na ni miezi sita/saba iliyopita tulikuwa majimboni kuomba kura, Mheshimiwa Mbunge analifahamu vizuri jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaelekeza wataalamu Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuendana na vipaumbele vya Mheshimiwa Mbunge tunapoenda kutekeleza ukamilishaji wa maboma hayo ili yakatoe tija katika huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ilikuwa nadra sana kwa vituo vyetu vya afya kuwa na *digital ultrasound*, *digital x–ray*, lakini kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameifanya nchi hii, sasa hivi unakwenda mpaka vijijini unakutana na *ultrasound*, unakutana na *digital x-rays* ambazo zinafanya kazi za upimaji. Kwa hiyo, tunaendelea kuongeza vifaa, tunawasiliana na wenzetu Wizara ya Afya ili *MSD* washushe vifaa katika zahanati zetu, vituo vyetu vya afya na vikatoe tija ya huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani ilikuwa unafata huduma hizi wilayani, lakini sasa hivi zinapatikana katika vituo vya afya vya kimkakati kote nchini, na tutaendelea kushusha vifaa kuhakikisha huduma bora zinaenda kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Chatanda, swali la nyongeza.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kunipa niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa kwenye kampeni Jimbo la Isimani nilikutana na hoja ya kutokamilika Kituo cha Afya Migoli. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kupelekea fedha ili waweze kukamilisha kituo hicho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mary Chatanda, Mwenyekiti UWT Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mama Mary Chatanda, tumemshuhudia kwenye kampeni akiwasisitiza wananchi wa Jimbo la Isimani kwanza kumpigia kura Mbunge wao na

ataendelea kulitetea jimbo lile na nimepata wivu mkubwa kwa maana ya kwamba tayari Jimbo la Isimani lina Waheshimiwa Wabunge wawili, ili waweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Migoli tumekitengea fedha katika bajeti ya mwaka 2026/2027 shilingi milioni 300 ili ziende zikakamilishe miundombinu katika kituo hiki cha afya. Nimhakikishie Mama Chatanda pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Isimani, tutaendelea kuwapa ushirikiano wa dhati kuona fedha hizi ambazo Serikali imeelekeza zinaleta tija na kutoa huduma tarajiwa katika kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Mwaka jana kabla ya kuvunja Bunge tulikaa na Wizara ya TAMISEMI kuhusu umaliziaji wa majengo ya zahanati ya jengo la Zahanati ya Mwanchimweo na jengo la Zahanati ya Sarakwa, wakakubali kwamba watatoa hizo fedha. Kipindi hiki nimekuja wakasema kabla ya mwaka kufungwa fedha zitatoka.

Sasa ni lini hizi fedha zitatoka, ninaona kesho kutwa tu msimu wa bajeti iliyopita unaisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Getere, mzee wa taarifa fupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Getere, mpango wa Serikali ni kukamilisha maboma yote ya zahanati na

yakatoe huduma kwa wananchi. Tunaanza kujenga kwa awamu, na awamu hii Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imeainisha zaidi ya maboma 1,841 ili kuhakikisha kwamba yanakwenda kutengewa fedha na kuanza ujenzi. Mheshimiwa Getere nikuhakikishie na Wanajimbo, tutakupa ushirikiano wa dhati kuhakikisha kwamba zahanati hizo ulizoziainisha zinakwenda kukamilika na kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikiuliza maswali hapa kila mara kwamba ni lini Serikali inaweza ikatusaidia vituo vya afya ama zahanati, lakini siku hii ya leo nimekuja kuishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan namna ambavyo ni sikivu. Imetuletea fedha kwenye Wilaya ya Rungwe kwa ajili ya vituo vya afya: Kisondela, Suma, Kinyala na Nkunga, imeleta fedha shilingi bilioni 2.5. Hivyo, ninatoa shukrani nyingi sana kwa usikivu huo kwa maana wananchi walio wengi wanakwenda kupona hasa upande wa wanawake na watoto, lakini na wananchi wote kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali, Hospitali ya Makandana tunashukuru mlituletea fedha nyingi sana, limejengwa jengo la ghorofa ambalo ni la mfano pale, limebaki kidogo tu kukamilika.

Sasa je, ni lini Serikali itatuletea fedha hizo kidogo ili tuweze kumalizia hospitali ya Wilaya ya Makandana ya Tukuyu Mjini? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fyandomo kama ambavyo ameliuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge aliibua suala hili katika Bunge lililopita, Bunge lako Tukufu na Serikali sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilichukua suala hilo kwa uzito mkubwa na ikatenga fedha kwenda kukamilisha miundombinu katika vituo hivyo vya afya ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameviainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishamaliza ng'ombe bado mkia, kwa hiyo, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge kwa ushirikiano wa dhati tutaendelea kutenga fedha kumalizia yale maeneo madogo yaliyobakia ili sasa yakatoe huduma bora kwa wananchi wetu na hasa akinamama wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Vingunguti yenye wakazi 70,000 na kata ambayo wakazi wake ni wa hali ya chini kabisa na hawana uwezo wa kwenda kupata matibabu katika vituo vya *private*.

Sasa swali langu kwa Serikali, ni lini mtatenga fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha afya ndani ya Kata ya Vingunguti ili hata hao wananchi wa Vingunguti waweze kupata huduma iliyo bora? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnesta Kaiza, Mbunge wa Jimbo la Segerea na ninampongeza Mheshimiwa Agnesta kwa kupigia kura ya ndiyo Bajeti ya Serikali kwa maana ya kwamba amekubali Serikali iendelee kupeleka fedha katika Jimbo la Segerea ili kwenda kujenga na kukamilisha miundombinu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya ziara katika Jimbo la Segerea na ninamwelekeza Mkurugenzi kupitia Bunge lako Tukufu, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kufika katika Kata ya Vingunguti na kuanza kutenga fedha, kuanza kutenga eneo kama vile ambavyo tulitenga katika Kituo cha Afya cha Buguruni ili tuhakikishe kwamba tunaanza ujenzi mara moja, na majimbo ya mijini, Ofisi Waziri Mkuu, TAMISEMI inatambua idadi kubwa ya watu, kwa hiyo, hatuna shaka katika hilo. Tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha kwamba tunajenga kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea swali linalofuata. Mheshimiwa Mary Daniel Surati, Mbunge wa Serengeti, sasa aulize swali lake.

Na. 688

**Kuimarisha Huduma za Afya kwa Waathirika wa Wanyamapori**

**MHE. MARY D. SURATI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha huduma za afya kwa wananchi wanaoathiriwa na wanyamapori Serengeti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Mary Daniel Surati na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua athari wanazozipata wananchi wanaoishi au kufanya shughuli za kijamii karibu na hifadhi zenye wanyamapori ikiwemo Serengeti. Aidha, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wananchi kuchukua tahadhari na kutoa taarifa kwenye mamlaka zinazohusika na hifadhi dhidi ya wanyama hatari kama tembo, simba, chui na fisi kipindi wanapotoka nje ya hifadhi na kuingia kwenye makazi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa pili ni ufuatiliaji wa karibu *(surveillance)* inayofanyika kwa wanyamapori ambapo Serikali kwa kushirikiana na wadau *Frankfurt Zoological Society* na *Grumeti Reserves*, imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa wanyama katika maeneo ya pembezoni mwa hifadhi na kuchukua hatua ya kuwarudisha wanyama hatari pindi wanapotoka nje ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa tatu ni kuimarisha huduma za afya kwa kujenga au kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, vituo vya afya pamoja na zahanati ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi pamoja na kuwahudumia wahanga walioshambuliwa na wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Daniel Surati, swali la nyongeza.

**MHE. MARY D. SURATI.** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi ninashukuru pia kwa majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na ninakiri kupokea ushirikiano wa dhati kutoka katika ofisi yake, na hivi punde siku si nyingi, tutakuwa tunaenda kufungua takribani zahanati zetu saba na hii ni kwa sababu ya msaada mkubwa ambao nimepewa na Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la msingi, kwa kuwa nimeridhika na majibu yaliyotolewa, ni lini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atafika jimboni Serengeti ili pia akajionee hali halisi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mary Daniel Surati na tunapokea pongezi alizozitoa kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kumpa ushirikiano na kwa kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, nitafika jimboni kwake ili kuhakikisha tunasisitiza maendeleo na kuamsha ari kwa wananchi kuona Serikali inavyowajali katika kupeleka maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, swali la nyongeza.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi ninaipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ambazo zinaendelea za kuboresha huduma za afya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kakonko tuna Kituo cha Afya cha Nyanzige ambacho kiko katika Kata ya Nyamtukuza. Katika kituo hiki cha afya ilitokea changamoto ya ardhi kutitia na kusababisha nyufa katika baadhi ya majengo ya kituo hiki cha afya na hivyo ikalazimika kusitisha kutumia baadhi ya majengo ikiwa ni pamoja na wodi za kulaza wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu jitihada zinaendelea katika halmashauri, lakini nguvu bado ni ndogo, je, Serikali Kuu iko tayari kutenga fedha ya dharura ili kuhakikisha sasa tunarekebisha tatizo hili na kufanya huduma ziendelee vizuri katika Kituo hiki cha Nyanzige? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Alan, Mbunge wa Jimbo la Kakonko na nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, hajachoka kuwapambania Wana-Kakonko na juhudi zake zinaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, na kupitia Bunge lako Tukufu, ninamwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri, afike kwenye maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaainisha kwanza na kuweza kufanya tathmini, na awasilishe andiko rasmi Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ili tuweze kuchukua hatua za dharura kuona namna ya kwenda kurekebisha miundombinu hii na iweze kutoa huduma tarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Eric James Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kuniona, nina swali moja tu dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha afya cha Kakobe kiliungua kwa moto na kwa sababu hiyo majengo kadhaa yaliharibiwa, lakini mpaka leo hakijafanyiwa ukarabati. Je, Serikali iko tayari kufika kituo hiki cha afya kujionea hali halisi na kufanya ukarabati ikiwezekana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la kaka yangu Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutafika katika kituo hicho cha afya ili tuweze kujionea miundombinu iliyoharibika na kutenga fedha katika mfuko wa dharura kuona tunaendelea kutoa huduma kwa wananchi wetu. Mheshimiwa Mbunge na Wana-Buchosa, ninawahakikishia tutafanya ziara katika jimbo lako na kuona namna ya kuamsha ari ya maendeleo katika jimbo lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Isack Copriano, swali la nyongeza.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anakumbuka nilimletea mezani suala la kuungua kwa kituo changu cha afya kule

Ngaruka. Je, ni lini Serikali basi itapeleka angalau fedha ili angalau irudishe hali ya kituo hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Isack na nianze kwa kumpongeza kwa kufuatilia miundombinu iliyopata athari ya moto katika jimbo lake pamoja na majimbo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi Waziri Mkuu, TAMISEMI inapokea taarifa kila baada ya dakika moja, kila baada ya saa, kufuatia mambo mbalimbali yanayotokea hasa haya majanga ya moto katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumeshaanza kuchukua hatua za dhati kwa kushirikiana na halmashauri yako ili kuhakikisha kwamba miundombinu ambayo imepata athari, tunaishughulikia kwa wakati na kupeleka fedha ambazo zitaenda kurekebisha miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, sasa ulize swali lake.

Na. 689

**Udhibiti wa Watumishi wa Afya na Elimu Kuhama Toka Vijijini**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti wimbi kubwa la watumishi wa sekta ya afya na elimu kuhama kutoka vijijini kwenda mijini baada ya kuajiriwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya watumishi wa sekta ya afya na elimu kuhama kutoka vijijini kwenda mijini mara baada ya kuajiriwa, hali inayosababisha kuwepo kwa upungufu wa watumishi katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti hali hiyo, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwemo matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya *e-Uhamisho* na *e-Msawazo* ambayo husaidia kudhibiti uhamisho holela kwa kuzingatia mahitaji halisi ya watumishi katika maeneo husika. Aidha, kupitia udhibiti huo, watumishi wa ajira mpya hutakiwa kutumikia katika vituo vyao vya kazi kwa muda usiyopungua miaka mitatu kabla ya kuomba uhamisho, isipokuwa kwa sababu maalumu ambazo zitathibitishwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali imeimarisha udhibiti wa utoaji wa vibali vya uhamisho kupitia mamlaka zilizokasimiwa jukumu hilo kama vile Ofisi za Wakuu wa Mikoa kwa uhamisho wa watumishi ndani ya mkoa, lakini Ofisi za Wakuu wa Wilaya kwa uhamisho wa watumishi ndani ya halmashauri husika ili kuhakikisha uwiano wa watumishi unabaki sawa kati ya vijijini na mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kazi vijijini kwa kujenga nyumba za watumishi,

kuboresha huduma za maji, umeme, mawasiliano pamoja na kutoa motisha mbalimbali kwa watumishi wanaofanya kazi katika maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tamima Haji Abass, swali la nyongeza.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia posho maalumu wafanyakazi wa sekta ya afya na elimu wanaopelekwa maeneo ya pembezoni kufanya kazi hasa ukizingatia wanawake kwa vile ndiyo kwanza wanaajiriwa wanakuwa wanapata changamoto nyingi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum kwa uchapakazi wake, anawasemea sana wananchi wa Tanzania na wanawake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza Serikali inatambua wapo watumishi wa sekta ya afya, sekta ya elimu na watumishi wa sekta nyingine ambao wanafanyakazi katika mazingira magumu ya vijijini na pembezoni mwa nchi yetu. Serikali imekuwa ikiboresha mazingira ya kazi kwanza kwa kuhakikisha tunaendelea kujenga nyumba za watumishi ili watumishi wakifika maeneo hayo wasipate shida ya kupata maeneo ya kuweka makazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili Serikali imeendelea kuboresha posho za watumishi kwa mujibu wa taratibu za utumishi wa umma ili kuendelea kuwapa motisha na kuhakikisha kwamba wanafanyakazi katika mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea na hivi sasa tunaendelea kufanya mazungumzo Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, lakini Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kuona mpango mzuri zaidi wa kuboresha motisha kwa watumishi hususan wanaofanyakazi pembezoni mwa nchi na hapo tutakapokubaliana kwamba inaweza ikafanyika jambo zuri zaidi tutahakikisha kwamba tunafanya utaratibu wa kuanza utaratibu wa kuwapa zaidi motisha watumishi katika maeneo hayo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Mtima, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nione je, Serikali haioni haja kuweka kipaumbele kwa watu wenye sifa wanaotoka katika maeneo hayo magumu ambao wanauzoefu wa kuishi maeneo yao ili kupunguza hilo zoezi la kuhamahama kutoka katika maeneo ya pembezoni kwenda mijini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Rashid Mtima amekuwa mdau muhimu sana kwenye masuala ya kuboresha sekta ya utumishi wa umma hapa nchini na mimi nimpongeze na nimhakikishie tu kwamba tutaendelea kumpa ushirikiano yeye katika jimbo lake kuhakikisha sekta ya utumishi wa umma inaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba katika maeneo mbalimbali wapo wananchi au wakazi wenye taaluma husika ambao wangeweza kufanya kazi katika maeneo hayo na Serikali imeendelea kuwapa fursa kufanya kazi katika maeneo mbalimbali kote nchini kwa sababu kimsingi kwa kuwa na watumishi ambao wanafanyakazi mbali na maeneo walikozaliwa pia inaendelea kujenga umoja wa nchi yetu. Kwa hiyo, siyo lazima sana mtumishi alipozaliwa afanye kazi eneo lilelile ni vizuri tukawa na mchanganyiko kwa maana ya kuwapa *exposure,* kuifahamu nchi yao, lakini pia kujenga uzalendo wa nchi yao kwa kufanya kazi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi ni kwamba mtumishi yeyote bila kujali amezaliwa eneo hilo au hajazaliwa eneo hilo akipangiwa kazi lazima tufuate utaratibu wa Serikali kwamba kwanza lazima akae angalau miaka mitatu na ikihitajika uhamisho lazima tujiridhishe kwamba ana sababu za msingi za kupata uhamisho kwenda maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kusimamia kuhakikisha maeneo ya mijini na vijijini yanaendelea kuwa na watumishi kwa usawa unaotakiwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Lucy Simirya Kombani. *(Makofi)*

Na. 690

**Upanuzi wa Shule ya Msingi Kilongo**

**MHE. LUCY D. S. KOMBANI K.n.y. MHE. SHEILA E. LUKUBA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga shule mpya au kuongeza madarasa katika Shule ya Msingi Kilongo, Kata ya Kihonda kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sheila Edward Lukuba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikijenga shule mpya au kuongeza miundombinu katika shule zilizopo ili kuendana na ongezeko la wanafunzi katika shule za msingi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitano mfululizo mwaka 2021/2022 – 2025/2026 Serikali imepeleka fedha katika Manispaa ya Morogoro shilingi bilioni 3.65 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya tano za msingi, vyumba vya madarasa 58, matundu ya vyoo 139, nyumba moja ya mwalimu, bweni moja, uzio na matundu ya vyoo 12 yaliyojengwa katika Shule ya Msingi Kilongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 740 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 13 vya madarasa, matundu 200 ya vyoo na ukamilishaji wa vyumba 15 vya madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa Shule ya Msingi Kilongo ina idadi kubwa ya wanafunzi na kutokana na wingi wa wanafunzi uliopo shule hii inahitaji kugawanywa. Hivyo, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imetenga eneo katika Mtaa wa Mlimani lenye ukubwa wa takribani ekari tano ili kujenga shule mpya ya msingi ambayo itapunguza msongamano katika Shule ya Msingi Kilongo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Simirya Kombani, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY D. S. KOMBANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nitauliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tayari eneo limeishapatikana kwa ajili ya ujenzi wa shule hii, je, Serikali haioni umuhimu wa kuipa kipaumbele katika mpango wake wa ujenzi wa shule ili kuwanusuru wananchi wa Kata ya Kihonda?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Jimbo la Morogoro Kusini lina changamoto kubwa sana kwenye shule za msingi hasa madarasa mengi ya shule hizi kuwa yamebomoka na pia sakafu za shule ile ina vumbi tena zile za *powder,* kitu ambacho ni hatarishi sana kwa wanafunzi hawa. Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kuwanusuru wanafunzi hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Lucy Kombani, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Morogoro kwa uchapakazi wake na kwa hakika anawasemea vyema sana Wananchi wa Mkoa wa Morogoro na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafahamu kwamba katika Kata ya Kihonda na katika shule hii ya Kilongo, wanafunzi ni wengi na tayari tulishaanza taratibu za kutafuta eneo ili tuweze kujenga shule nyingine ya mkondo B ili wanafunzi waweze kupunguzwa kwenye shule hii ya Kilondo na kwenda kusoma kwenye shule nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa navyoongea tayari Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro tumepata eneo lenye ukubwa wa ekari tano na tumeanza taratibu za kibajeti ili tuweze kutoa kipaumbele na kujenga shule hii mapema iwezekanavyo wanafunzi waweze kuanza kusoma katika shule hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kombani kwamba suala hilo litafanyiwa kazi na tutatoa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunafahamu kweli tunazo shule nyingi kongwe na Serikali imeendelea kwanza kujenga shule nyingine mpya, maeneo mengine tumeendelea kuboresha kwa kujenga madarasa mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa elimu msingi tumetumia mpango wa *BOOST* na tumejenga madarasa mapya, tumejenga shule mpya kote nchini na kwa upande wa sekondari tumetumia mpango wa *SEQUIP* na tumeendelea kukarabati shule na kujenga shule mpya za sekondari kote nchini.

Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunafahamu kwamba katika Jimbo la Morogoro Kusini na maeneo mengine kote nchini ziko shule chakavu na mpango huo kila bajeti ya mwaka wa fedha tunahakikisha tunapeleka fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshafanya tathmini tunazo jumla ya shule 11,000 chakavu; za msingi 10,595 na sekondari 405 ambazo kwa ujumla wake ili kuzikarabati tunahitaji angalau shilingi trilioni 1.3. Hivi sasa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tunaendelea na mawasiliano na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji na Wizara ya Fedha ili kuona namna ya kupata fedha kwa awamu kwa ajili ya kufanya ukarabati wa shule hizi na nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaipa kipaumbele pia shule hii ya Morogoro Kusini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; wananchi wa kata ya Makongolosi wameanza ujenzi wa sekondari mpya kwenye Kijiji cha Mwaoga sambamba na wananchi wa Kata ya Matundasi kwenye Kijiji cha Itumbi pamoja na wananchi wa Kata ya Kasanga na tayari shule hizi zipo kwenye hali ya maboma, je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili maboma haya yakamilike na shule hizi zikamilike na huduma ya elimu iweze kutolewa kwenye kata hizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Chunya na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tu kwamba tunafahamu nikupongeze sana kwa kazi nzuri ya kuhamasisha wananchi na niwapongeze wananchi wa Chunya kwa kuchangia nguvu zao pamoja na halmashauri kuanza ujenzi wa shule hizo za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya mpango kwanza wa kufanya tathmini ya uhitaji wa shule mpya katika kata zilizopo, lakini pili kwa kutekeleza Sera ya Elimu ya mwaka 2014, Toleo la 2023 ambapo Januari, 2028 tutakuwa na *double coach,* wanafunzi wa darasa la sita na darasa la saba mwaka 2027 wote kwa pamoja wataanza kidato cha kwanza Januari, 2028.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishatoa maelekezo kwa wakurugenzi wote wa halmashauri zetu kuwasilisha shule ambazo zimeanza kujengwa na hazikamilika au maeneo ambayo yanahitajika kujenga shule ambazo zitaweza ku-*absorb* wanafunzi wa Januari, 2028 waweze kuwasilisha Ofisi ya Waziri, TAMISEMI ili tuweze kufanya taratibu za kibajeti kwa ajili ya kujenga shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini Mheshimiwa Mbunge halmashauri watawasilisha na sisi tutaoa kipaumbele

wakati wa ujenzi wa shule hizo ili Januari, 2028 ziweze kuwa sehemu ya shule ambazo zinachukua wanafunzi wa kidato cha kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mbulu Vijijini tuna Shule ya Msingi Mangisa ambayo iko karibu kabisa na Bwawa la Umwagiliaji la Mangisa na sasa ile shule imeanza kutitia na haiku salama kabisa kwa ajili ya watoto/wanafunzi, je, Serikali ina mpango gani wa kuinusuru ile shule na wanafunzi wale ili kupata shule mpya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimpongeze Mbunge wa Mbulu Vijijini, Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas kwa ufuatiliaji. Nafahamu ziko shule katika Jimbo la Mbulu Vijijini ikiwemo hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hizo ambazo zinahitaji ukarabati, zinahitaji kujengwa miundombinu ama kuongezewa miundombinu mingine. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tumefanya tathmini na tunaendelea na taratibu za kibajeti na wakati wa utekelezaji tutaipa kipaumbele shule hiyo ili iweze kufanyiwa maboresho na kunusuru mazingira ya wanafunzi katika masomo yao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Neema Majule, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu Shule ya Ipagala A iliyoko Kata ya Makole, *center* kabisa ya hapa mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule hii ni kubwa sana, yaani ina eneo kubwa sana, lakini kuna eneo kubwa limebaki ambalo lingeweza kutoa shule ya sekondari, je, Naibu Waziri upo tayari kuambatana na mimi kwenda kuliona hili eneo ili tuweze kupata shule ya sekondari *center* kabisa hapa mjini ili kuweza kuchukua watoto wengi zaidi hapa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Neema Majule, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma kwa uchapakazi na ufuatiliaji, lakini nikuhakikishie tu kwamba dhamira ya Serikali ni kuongeza miundombinu ya sekta ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule hiyo ya msingi ya Ipagala A tutakwenda kufanya ufuatiliaji, kwanza niko tayari kuambatana na wewe kwenda kufanya ziara katika eneo hilo. Lakini nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma katika kutekeleza yale maelekezo ya kuwasilisha maeneo yanayohitaji kuongezewa mindombinu ya shule za sekondari, waende kulifanyia tathmini eneo la Shule ya Msingi ya Ipagala A ili ikiwezekana waweze kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa ajili ya hatua za ujenzi zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi, swali la nyongeza.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, katika Jimbo la Katoro kuna shule moja ya msingi inatwa Shule ya Msingi Katoro inapokea watoto wenye changamoto yaani tuseme mnatumia lugha gani yaani wenye mahitaji maalumu. Watoto wale wanakaa/wanaishi palepale shuleni, lakini wanakaa bweni moja yaani wa jinsia ya kiume na jinsia ya kike.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha inaongeza sehemu za kulala ili itofautishe hao watoto wa kiume na wa kike walale sehemu tofauti? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi, Mbunge wa Jimbo la Katoro alikwishawasilisha taarifa ya shule hiyo ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya Katoro na mpango wa Serikali ambao umeendelea kutekelezwa ni kujenga *hostel* au mabweni kwenye shule zote zenye mahitaji maalumu na hususan watoto ambao wana ulemavu wa aina tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tu nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga bajeti, kufanya tathmini ya mahitaji ya *hostel* au mabweni na tutaendelea kujenga na tutaipa kipaumbele pia shule hiyo ili tuboreshe mazingira ya wanafunzi kusoma na kujifunza katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fagason Nkingwa, swali la nyongeza.

**MHE. FAGASON A. NKINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Mbogwe linazo shule nyingi sana ambazo ni za zamani, shule zimekuwa chafu, chakavu ikiwepo Shule ya Masumbwe, Lulembela, Ikunguigazi; je, ni lini Serikali italeta fedha kwa ajili ya kuhakikisha inatengeneza shule hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, shule za Jimbo la Mbogwe kwa Mheshimiwa Mbunge Fagason ni moja ya shule ambazo zimetambuliwa, kwa sababu tulipita kwenye halmashauri zote ikiwepo Halmashauri ya Mbogwe tukatambua shule chakavu za msingi jumla 10,595.

Naomba nimthibitishie kwamba shule hizo ambazo amezitaja ambazo ni kongwe na chakavu ni miongoni mwa shule 10,595 ambazo tutakwenda kuzitengea bajeti kwa awamu ili kuhakikisha kwamba tunaifanyia matengenezo ama tunajenga upya shule nyingine ili kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 691

**Ujenzi wa Shule Mpya za Sekondari Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa shule nne mpya za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Nanyumbu ina kata 17 na shule za sekondari 22 ambapo hakuna kata ambayo haina shule. Kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 - 2025/2026 Serikali ilipeleka shilingi bilioni 5.56 katika Halmashauri ya Nanyumbu kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya sita za sekondari, madarasa 107, mabweni 13, maabara 10, matundu ya vyoo 78 na ukarabati wa madarasa tisa na *hostel* mbili. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 560.55 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Kata ya Kilimahewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 380 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa tisa, nyumba za walimu wawili, matundu ya vyoo mawili na ukamilishaji wa maabara mbili katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya kuwapambania watoto wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo milioni 560 zimeshawasili ndani ya jimbo langu namshukuru sana na naishukuru sana ofisi hii na naomba niwahakikishie kilio cha wananchi wa Kijiji cha Misawaje, Msinyasi, Nachura na Kutofora kinakwenda kumalizika tunamshukuru sana Rais wetu. *(Makofi)*

Sasa nina ombi moja, naiomba sana Wizara…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya, kidogo naomba usogeze kisemeo.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi moja tu kwa Wizara, tunazo tarafa nne zina kidato cha tano na sita, tunayo tarafa moja ya Nakopi haina mkondo wa kidato cha tano na sita, je, Wizara haioni haja katika mwaka ujao wa fedha ikapeleka fedha ili tarafa ile Nakopi kwenye Kata ya Michiga ikapata mkondo wa kidato cha tano na cha sita ili kukamilisha tatizo hilo katika jimbo langu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu kwa namna ambavyo anawawakilisha ipasavyo wananchi wa Jimbo la Nanyumbu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika wananchi wa Nanyumbu wamepata Mbunge jembe, mchapakazi na mfuatiliaji kweli kweli. Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu kwamba Serikali tutaendelea kukupa ushirikiano kuhakikisha kwamba tunaboresha mazingira ya sekta ya elimu katika Jimbo la Nanyumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nipokee pongezi zake nyingi alizozitoa kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na nihakika kwamba Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa ambayo haihitaji *lens* wala miwani kuona na kwa hakika Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anastahili maua yake kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge moja ya mipango ya Serikali ni kuendelea kuongeza shule za kidato cha tano na sita katika maeneo yote yanayokidhi vigezo vya kuwa na shule hizo. Tunajua tunazo shule za kidato cha tano katika tarafa, lakini ziko tarafa hazina shule hizo, tutahakikisha Mheshimiwa Mbunge katika taarifa ambayo umeitaja tunaipa kipaumbele kwa kadiri ya bajeti zetu ili tuweze kujenga madarasa ya kidato cha tano na sita. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Kwa kuzingatia mchango mkubwa ambao wameonesha wananchi wa mitaa ya Nyakenene, Nyasebe na Itununu kwa kujenga maboma ya madarasa na jengo la utawala kwa ajili ya sekondari mpya ya Gamasara, ili kuweza kupunguza umbali mrefu ambao unawakabili wanafunzi wanaotembea kwenda kutafuta elimu kwenye Shule ya Sekondari ya Nyakisese na Nyandoto na kwa kuzingatia hali halisi ya maisha hamna mzazi ambaye anaweza ku-*afford* zaidi ya shilingi 5,000 kwa siku kwa bodaboda mwanafunzi kwenda shuleni ambapo wanafunzi hao wanafika wakiwa wamechoka na kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujua nini mkakati Serikali wa kuharakisha ukamilishaji wa miundombinu ya maboma hayo ambayo wananchi wamejitolea kujenga ili sasa wanafunzi wa Mitaa ya Nyakenene, Itununu na Nyasebe, waweze kupata elimu kwa muda muafaka na bila kuchoka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimpongeze Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini, niwapongeze wananchi kwa kujitolea nguvu zao lakini pia na *support* ya Mbunge na halmashauri kuhakikisha wanajenga maboma.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kukamilisha maboma yote, kuwezesha wanafunzi kusoma karibu na makazi yao na hii itawezesha kuboresha uwezo wao kujifunza zaidi, lakini pia kuepusha changamoto wanazokutana nazo kutokana na kutembea umbali mrefu.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Esther Matiko, tutaipa kipaumbele kwenye bajeti zetu, kuhakikisha Serikali inapeleka fedha na kukamilisha maboma hayo ili wanafunzi wapate mazingira bora ya kusoma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaona mpo wengi ninaomba maswali mafupi.

Mheshimiwa Paschal Chinyele, swali la nyongeza.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jiji la Dodoma zipo kata tatu za Mbabala, Mkonze pamoja na Matumbulu ambazo mitaa yake ikiwemo Mtaa wa Chikoa katika Kata ya Mbabala, Mtaa wa Chikola Kata ya Matumbulu pamoja na Mitaa ya Chisichili, Goba pamoja na Chinyika katika Kata ya Mkonze; watoto wanaokaa katika mitaa hii wanalazimika kutembea umbali wa kati ya kilometa tano hadi 12 kufuata elimu ya sekondari, katika Shule za Sekondari za Wella pamoja na Mkonze.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inampango gani wakujenga shule katikati katika eneo la Mkonze ili watoto hawa waweze kufika kirahisi shuleni na hivyo kuepuka kutembea mwendo kufuata shule hizi nilizozitaja?

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, upo tayari tukimaliza Bunge twende na wewe ushuhudie watoto wanavyotembea mwendo mrefu kufuata elimu ya sekondari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jibu swali moja, kwa sababu ameuliza maswali mawili kwa pamoja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nijibu swali la Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mbunge wa Dodoma Mjini; kwanza, nimthibitishie kwamba mpango wa Serikali ni kujenga shule nyingine mpya za sekondari na hususani tunapoelekea kuchukua wanafunzi wa *double cohort* Januari 2028.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tayari tumetoa maelekezo kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuwasilisha maeneo yenye vigezo kwa ajili ya kujenga shule mpya, ama kuongeza madarasa katika shule zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo katika Kata hizi za Mkonze, Mbabala na Matumbulu, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kumuelekeza Mkurugenzi kwamba wafanye tathmini na ikiwa zinakidhi vigezo vya kujengewa shule kwa maana ya idadi ya wanafunzi katika eneo hilo wawasilishe Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI iingizwe kwenye mipango na tutahakikisha tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili niko tayari kushirikiana na wewe kwenye ziara kwa ajili ya kukagua miradi ya maendeleo katika Jimbo la Dodoma Mjini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, swali la nyongeza.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na ninapenda nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba siyo tu majengo ya sekondari, lakini hata hizi sekondari tulizonazo tunatamani kuwa na vifaa vya kutendea kazi katika hizi sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo sekondari moja ya Mindu, iliyopo Kata ya Mindu, Halmashauri ya Tunduru, sekondari ile haina hata *photocopy machine*, ni wazi kwamba wakitaka hata kuandaa mitihani ni lazima waende kata ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitamani kujua ni nini mkakati wa Serikali katika kuhakikisha tunapeleka vitendea kazi na *photocopy machine* katika hiyo sekondari ya Mindu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yatokane na swali la msingi.

Tunaendelea, Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Isaba, Kata ya Buruma na Kijiji cha Magunga, Kata ya Merwa na Kijiji cha Aliamsanga, Kata ya Bwiregi ni vijiji ambavyo vinauhitaji mkubwa sana wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali, je, lini Serikali itapeleka fedha ili kujenga sekondari katika vijiji hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa mujibu wa sera na miongozo yetu ya elimu sekondari, kwa sasa mpango wa Serikali ni kujenga shule za sekondari kwa kuzingatia kata na ikiwa kata ina wanafunzi wengi tunaweza kujenga shule nyingine ya sekondari ndani ya kata hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera, Mbunge wa Butiama, tumepokea ombi la kufanya tathmini katika maeneo ya vijiji hivyo na ikiwa vitakidhi vigezo vya kuwa na shule za sekondari na hasa kuzingatia umbali wa wanafunzi wanaosoma hapo, lakini pili idadi ya wanafunzi basi Serikali katika mipango yake ya kibajeti tutawapa kipaumbele eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika imejitolea sana kujenga shule za sekondari kupitia mapato ya ndani.

Swali langu ninauliza, ni lini Serikali itaenda kuwashika mkono kumalizia shule hizo za sekondari zilizopo kwenye Halmashauri ya Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa kuunga mkono juhudi za wananchi na halmashauri katika ujenzi wa miundombinu ya elimu, ikiwemo ujenzi wa shule mpya. Nimthibitishie Mheshimiwa Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Tanganyika,

kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye bajeti na tutahakikisha shule hizo ambazo zimejengwa na nguvu za wananchi na halmashauri zinakamilishwa, aidha kwa mapato ya ndani, lakini pia kwa kutumia fedha za kutoka Serikali Kuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali la nyongeza.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru na niishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutujengea shule ya kisasa ya wasichana pale Simiyu.

Je, ni lini sasa Serikali itajenga uzio kwenye shule hii ili kuimarisha ulinzi kwa ajili ya wasichana hawa hasa tukizingatia kwamba ni watoto wa kike na lile eneo lipo wazi? Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimpongeze sana mama yangu, Mama Chenge kwa namna ambavyo amekuwa msemaji madhubuti sana wa Wananchi wa Mkoa wa Simiyu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu swali hili limeulizwa sana na akinamama kwa sababu wanajua zaidi umuhimu wa kuwa na usalama kwa watoto wetu, wiki iliyopita aliuliza Mheshimiwa Mary Chatanda, Mbunge na Mwenyekiti wa UWT, leo mama yangu Mama Chenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu na niwathibitishie kwamba Serikali inatambua na inathamini usalama wa wanafunzi katika shule zetu zote kote nchini, zikiwemo zile shule za mikoa 26 na hususani ikiwemo shule ya Mkoa wa Simiyu. Tayari Serikali imeendelea kutenga fedha kwa awamu kupitia Bajeti Kuu ya Serikali na tumeanza kujenga *fence* katika baadhi ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shule zile ni shule za mikoa na zipo katika halmashauri moja, lakini zinahudumia wanafunzi wa mkoa mzima, Serikali ilikwishatoa maelekezo na ninaomba nisistize kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwamba Makatibu Tawala wa Mikoa yote katika shule hizo za wasichana za mikoa, wakae na Wakurugenzi wa Halmashauri zote zilizopo ndani ya mikoa, waandae taratibu za kibajeti ili wachangie kuanza ujenzi wa *fence* hizo kwa sabau zile shule ni shule za mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo halmashauri zote ndani ya mkoa zianze kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi na wakati huo Serikali Kuu ikiendelea na taratibu za kibajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa *fence* hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Katiba na Sheria, swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Iramba Mashariki, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete.

Na. 692

**Ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mkalama**

**MHE. SALMA R. KIKWETE K.n.y. MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mkalama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji haki katika ngazi mbalimbali. Mpango huu unahusisha ujenzi wa majengo mapya pamoja na ukarabati wa majengo yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mkalama unatekelezwa kwa bajeti ya mwaka 2025/2026. Mradi huu ulikuwa ukamilike kabla ya mwezi Aprili, 2026. Hata hivyo, kutokana na sababu mbalimbali, mradi huu uliongezewa muda na sasa umefikia 60% na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza, niipongeze na kuishukuru Serikali kwa kujenga mahakama katika nchi yetu ya Tanzania na hata huo mradi ambao anauzungumzia Mheshimiwa Kishoa, kwa majibu ya Serikali amesema umekaribia 60%, tunaiomba Serikali utimize 40% zilizosalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nina maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, na mimi ninapenda kuishukuru Serikali, katika Jimbo la Mchinga kwenye Tarafa ya Mipingo, imejengewa Mahakama ya Mwanzo na mpaka sasa hivi Mahakama imekamilika. Watumishi watatu wameletwa pamoja na Hakimu mmoja yupo na tayari wanafanya kazi. Kwa kweli ni Mahakama nzuri na ni Mahakama za kisasa. Ahsante sana Serikali, ahsante sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ninataka kujua, je, ni lini katika jimbo langu la Mchinga kwenye Tarafa ya Mchinga,

tutapata Mahakama ya kisasa kama ilivyokuwa ya Mipingo, kwa sababu Mahakama iliyopo katika Tarafa ya Mchinga, Tarafa ya Nangaru na Tarafa ya Milola ni Mahakama za muda mrefu sana, ninataka kujua nini kauli ya Serikali? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Jimbo la Mchinga, kwa swali lake hili zuri, maswali yake ambayo lengo lake ni kufuatilia upatikanaji wa haki katika jimbo analotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita, imefanya uwekezaji mkubwa sana katika mhimili wa Mahakama. Kwa takribani miaka mitano, Serikali imekuwa ikitekeleza mradi huu mahsusi kabisa wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama, ambapo Serikali imetumia shilingi bilioni 524.9 kwa ajili ya kuboresha majengo ya mahakama lakini siyo majengo peke yake bali pia hata mifumo ya TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyozungumza kwa wakati huu katika mhimili wa Mahakama kwa mara ya kwanza unatumia teknolojia ya TEHAMA ambapo wakili anaweza akafungua shauri kimtandao, shauri likafuatiliwa na mashahidi wakatoa ushahidi na kuhudhuria shauri kimtandao na hukumu ikatoka pia kwa njia ya kimtandao. Hii ni *legacy* ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na mapinduzi yote hayo tunaona majengo mbalimbali ya mahakama, kuanzia Makao Makuu ya Mahakama, Mahakama za Rufani, *High Court,* lakini Mahakama za Wilaya pamoja na Mahakama za Mwanzo, zimekuwa zikijengwa na ndio maana hata katika jimbo hili la Iramba Mashariki, Wilaya ya Mkalama, tayari wilaya hii inajengewa Mahakama ya Wilaya na utakapofika mwisho wa mwezi huu tayari

mahakama hii ya Wilaya itakuwa imekamilika kwa ajili ya kuanza kutoa huduma hizi za haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Salma Kikwete, katika jimbo lako umeeleza na umetoa pongezi, ninaomba nizipokee kwa niaba ya Serikali kwa kazi ya ujenzi wa Mahakama hii ya Mwanzo, lakini ninaomba nikuhakikishie kwamba Serikali inaendelea kutoa fedha kupeleka katika mhimili wa Mahakama kwa ajili ya kuendelea kuboresha miundombinu hii muhimu kabisa ya mahakama kwa ajili ya upatikanaji wa haki na tarafa hii ya Mchinga, itafikiwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Mahakama hii ya Mwanzo inajengwa ili wananchi waweze kupata huduma bora za upatikaniaji wa haki, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Tabora Mjini lina Mahakama za Mwanzo kwenye Kata ya Gongoni yaani Mahakama ya Mjini, lakini kwenye Kata ya Isevya, mahakama hizi zimechakaa kwelikweli, hivyo kuleta hofu hata kwa wale wanaokwenda kusikiliza kesi zao, kwamba mahakama hizi zinaweza zikawadondokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu nipate kauli ya Serikali, nini mpango wa Serikali kukarabati mahakama hizi ambazo zipo tangu wakati wa mkoloni ili wananchi waweze kupata huduma bora kwenye sehemu bora?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge wa Tabora Mjini kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwasemea wananchi

wake na hasa sasa kwa sababu anahimiza uimarishaji wa upatikanaji wa haki katika jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake hili, kwamba Serikali ya Awamu ya Sita, inafanya uwekezaji mkubwa sana katika mhimili wa Mahakama. Kama nilivyotangulia kusema katika kipindi cha miaka mitano tu ya Serikali ya Awamu ya Sita, tayari imeshatoa shilingi bilioni 524.9 kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefanya hivyo kwa kufika kwenye maeneo mbalimbali ya nchi, siyo tu kujenga Mahakama mpya, lakini pia kufanya ukarabati katika majengo yale ambayo yamechakaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo la Serikali ni kuendelea kuimarisha mhimili huu wa Mahakama na Mahakama itafika katika jimbo hili la Tabora Mjini kwa ajili ya kujenga *Primary Court* (Mahakama ya Mwanzo) katika kata aliyoitaja. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika mwaka wa fedha unaokuja Mahakama itafika kwa ajili ya kujenga Mahakama hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninatambua mnajadili mambo ya msingi, ninaombeni mjadili kwa sauti ya chini ili maswali ya wananchi yasikike na Serikali iweze kutoa majibu sahihi, tujadili kwa sauti ya chini.

Mheshimiwa Margaret Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la Mahakama ya Mwanzo Wilayani Urambo lipo katika hali mbaya sana kutokana na kujengwa kabla ya Uhuru na kila mvua inaponyesha huzungukwa na maji na

kusababisha hali ngumu sana kwa wanaofanya kazi pale ikiwemo ni pamoja na Mahakimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itatujengea jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nirudie, wakati Mbunge anauliza swali tuwe watulivu ili Serikali iweze kusikia.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwanza kumpongeza Mheshimiwa Margaret Sitta, kwa hakika amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu na wa mara kwa mara kuhakikisha kwamba wananchi wake katika jimbo lake wanapata huduma bora kabisa za haki na hasa kwa kupata majengo bora kwa ajili ya huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Margaret Sitta tayari nilishazungumza naye na nikamueleza kwamba tayari Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa maelekezo kwetu sisi kwamba, Wizara ya Katiba na Sheria, tushirikiane pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, pamoja na Wizara ya Fedha, kuhakikisha kwamba Mahakama hizi za Mwanzo ambazo zipo karibu zaidi na wananchi na zinasaidia sana katika upatikanaji wa haki kwa Watanzania zinajengwa katika kata zote za Tanzania hii Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutoa fedha katika mhimili wa Mahakama kwa ajili ya kutekeleza maelekezo haya mahsusi kabisa ili tuweze kufika katika kata hii aliyoitaja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama hii ya Mwanzo ili wananchi wake waweze kupata huduma bora za upatikanaji wa haki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mecktridis Mdaku, swali la nyongeza.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, wananchi wa Jimbo la Malinyi wamekuwa wakikosa haki zao za msingi na wamekuwa wakifuata Mahakama umbali mrefu na kwa gharama kubwa. Je, ni lini Serikali itawapa wananchi wa Malinyi haki zao za Kikatiba na kwa gharama ndogo kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Malinyi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri hii anayoifanya ya kupaza sauti yake kwa ajili ya wananchi wa Malinyi kupata huduma bora za upatikanaji wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba Serikali ya Awamu ya Sita, inafanya uwekezaji mkubwa sana kuhakikisha kwamba inaimarisha mhimili huu wa Mahakama kwa kufanya ukarabati na ujenzi wa majengo ya Mahakama. Mpaka wakati huu Mahakama imehakikisha kwamba katika wilaya 136 kati ya wilaya 139 huduma za Mahakama ya Wilaya zinapatikana, lakini katika hizi wilaya tatu tayari ujenzi wa Mahakama unaendelea. Kwa hiyo, mwisho wa siku tunatarajia mpaka mwaka huu unakamilika wilaya zote 139 zitakuwa zinapata huduma ya Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo huduma za kimahakama zinapatikana, Mahakama za Wilaya lakini kwa majengo ambayo ni ya kuazimwa Serikalini na ndiyo maana mahakama inatumia fedha nyingi kuhakikisha kwamba inajenga majengo ya Mahakama katika wilaya hizi kwa kutumia fedha ambazo zinatoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge umeeleza kwamba majengo ni chakavu na kuna uhitaji na kwa sababu mahakama inahuisha mpango wake wa tatu wa ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama

nikuhakikishie kwamba lengo la Mahakama ni kufika katika wilaya hiyo na kujenga jengo ambalo litatoa huduma bora kwa Watanzania za upatikanaji wa haki, ahsante,

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa jengo la Mahakama Wilaya ya Hanang?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Asia Halamga kwa uwakilishi bora kabisa katika Jimbo lake hili la Hanang na hasa kwa kupaza sauti yake kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora za upatikanaji wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya hii ya Hanang tayari Mahakama imefika na kuanza ujenzi wa Mahakama ya Wilaya na jengo hili la Mahakama ya Wilaya limefika katika hatua nzuri. Tunatarajia katika mwaka wa bajeti unaofuata fedha zitapatikana kwa ajili ya kuhakikisha jengo linakamilika ili wananchi wako waweze kupata huduma bora za upatikanaji haki katika majengo bora kabisa ya kimahakama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la Mahakama ya Hedaru lililoko Wilaya ya Same ni chakavu sana. Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati katika jengo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Zuena Bushiri kwa swali lake hili zuri sana ambalo linalenga kufuatilia upatikanaji wa haki katika Wilaya hii ya Same na naomba nimhakikishie kwamba Serikali inaendelea kuimarisha mhimili huu wa Mahakama kwa kupeleka fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati na ujenzi wa majengo ya mahakama ikiwa ni pamoja na miundombinu mingine kama nilivyotangulia kusema miundombinu ya ki-TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu tayari kazi hii ya ujenzi wa miundombinu hii umeshaanza, miundombinu ya Mahakama na ujenzi unafanyika kwa awamu, ni dhamira ya Mahakama kufika katika Wilaya ya Same ili kuhakikisha majengo ya Mahakama ya Wilaya katika wilaya hii yanakuwa ni bora kwa ajili ya upatikanaji wa haki ulio bora zaidi kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, sasa aulize swali lake.

Na. 693

**Malipo ya Awali kwa Mkandarasi wa Barabara ya Sengerema - Nyehunge**

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza: -

Je, lini mkandarasi aliyeshinda kandarasi ya ujenzi wa Barabara ya Sengerema hadi Nyehunge atapewa malipo ya awali ili aanze kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Sengerema - Nyehunge amelipwa malipo ya awali ya 10% mwezi Machi, 2026. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kambi, mitambo na wataalamu kwa ajili ya kuanza kazi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Eric James Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa mambo makubwa mawili; jambo la kwanza ni kutoa shukrani nyingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa jambo hili kubwa ambalo limefanyika tangu Uhuru wa nchi yetu hatujawahi kuwa na barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninalo swali moja tu la nyongeza; barabara hii inasoma Nyehunge - Sengerema na kipande cha Kahunda kilometa 32. Inayojengwa ni Sengerema hadi Nyehunge; je, kipande hiki cha Nyehunge - Kahunda kilometa 32 kitakuwepo kwenye bajeti ya 2027/2028?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nipokee pongezi za Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Buchosa kwa niaba ya Serikali kwa kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaifanya katika sekta hii ya miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu swali lake la pili barabara hii inasoma Sengerema – Nyehunge - Kahunda. Kwa hiyo, tumeanza kwa awamu kutoka Sengerema hadi Nyehunge, lakini barabara imesanifiwa yote mpaka Kahunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande hiki cha Sengerema hadi Nyehunge kwa mujibu wa mkataba kitajengwa kwa miezi 28. Kwa hiyo, tuna uhakika baada ya kukamilisha kipande hiki ama kama hali ya kibajeti itaruhusu, Serikali mpango wake ni kuijenga barabara yote Sengerema - Nyehunge hadi Kahunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Buchosa kwamba lengo la Serikali ni kuifikisha hii barabara kwa kiwango cha lami kama ilivyosanifiwa hadi Kahunda, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali nyongeza.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na Mheshimiwa Deo Mwanyika mara kadhaa tumeweza kukuona Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri ameahirisha ziara mara mbili pale sehemu ya Barabara ya Itoni - Lusitu. Kwa hiyo, wananchi wana kero ya muda mrefu na wakati wote Serikali imetuhakikisha kwamba mkandarasi ameshalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa kuwa leo tunamaliza Bunge uko tayari Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi na Mheshimiwa Deo Mwanyika tukakaa na wewe tukapanga ziara ili tuweze kuwaeleza wananchi juu ya hatua zinazochukuliwa na Serikali juu ya kuamua kipande hiki cha Barabara ya Itoni-Lusitu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kamonga, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mkandarasi huyu ameshalipwa na ameshaelekezwa kurudi eneo la kazi ili aweze kuanza kazi, lakini pia ameshataarifiwa kwamba asipofanya hivo basi taratibu za kimkataba zitaanza kuchukuliwa kama hatarudi kwa muda ambao tumemwelekeza na hasa baada ya tutakapokuwa tumekutana na utawala wake kwa maana ya menejimenti ya juu kabisa ya huyo mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la kwenda maeneo hayo ya kutembelea hiyo Barabara ya Itoni - Lusitu nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tuko tayari ambapo tutatembelea hilo eneo na tutakutaarifu Mheshimiwa wa Ludewa na Mheshimiwa wa Njombe Mjini, Mheshimiwa Mwanyika. Kwa hiyo, tuko tayari nakuja kuwaeleza wananchi kwamba tumeshamlipa na mkandarasi ataanza kazi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abubakar Omari, swali nyongeza.

**MHE. ABUBAKAR A. OMARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza awali ya yote napenda kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutukumbuka Wana-Manonga na kutupatia barabara kuingiza kwenye mpango wa kutia lami barabara yetu kuu kutoka Choma – Ziba - Ndala mpaka Puge.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali sasa, ni lini mpango huu wa ujenzi unaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Manonga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii tutaenda kuijenga kwa awamu na tulishatoa maelekezo kwa wenzetu wa *TANROADS,* ilitangazwa kwanza, lakini ilishindwa kuanza. Nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba vile vipande tulivyoahidi kuvijenga, katika mwaka huu wa fedha tunaoendea hiyo barabara itatengenezwa ili kukamilisha ile ahadi ambayo tulikuwa tumeahidi na tumeipanga kwenye bajeti kuendelea na vile vipande ambavyo tulikuwa hatujaanza kuvifanyia kazi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fadhili Ngajilo, swali la nyongeza.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuniona ili niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niishukuru sana Serikali kwamba ilileta shilingi bilioni sita kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi ule wa *Bypass* ya Igumbilo - Kihesa ambalo ni jambo kubwa na mradi ule una thamani ya shilingi bilioni 41.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tuna changamoto kwamba mkandarasi amesimamisha kazi kwa muda mrefu na yeye mwenyewe pia anatudai zaidi ya shilingi bilioni tisa na shughuli pale zimesimama, ajira za vijana zimesimama ambazo zilikuwa zinajenga ule mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu, Mheshimiwa Naibu Waziri wewe umeshafika pale kwenye ule mradi umejionea mwenyewe. Ni lini sasa kauli ya Serikali itaelekeza kwamba mradi ule uanze kujengwa ili wananchi wa Iringa Mjini wawe na matumaini kwamba *bypass* ya Igumbilo - Kihesa itakamilika kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, bahati nzuri wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya ziara, mimi mwenyewe nilikuwepo na tumeitembelea ile barabara ambayo kwa sasa walau unaweza ukapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, na niungane na Mheshimiwa Mbunge Ngajilo ni moja ya barabara muhimu sana kwa sababu hakuna namna yoyote kama barabara itafunga ya kutoka Iringa kwenda pale chini. Kwa hiyo, hiyo barabara ndio mkombozi na tumesema hapa kwamba miradi yote ambayo ilikuwa imesimama, ama imekwama, ama inasuasua, baada ya kukamilisha hii miradi mikubwa, miradi kama hiyo ambao ni wa *Iringa bypass* ndio miradi ambayo tunaipa kipaumbele, tuna uhakika tutamlipa huyo mkandarasi ili arudi na aweze kujenga hiyo barabara kwa uharaka sana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kafiti Kafiti, swali la nyongeza.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kwa kuniona niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua nimesimama hapa Mheshimiwa Waziri anajua kabisa naulizia barabara gani. Barabara ya *Airport* - Kayenzi. Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikiuliza leo ni mara ya tatu, hebu leo toa kauli kwa Wana-Ilemela ili uwape matumaini juu ya Barabara ya *Airport* - Kayenzi. Nafahamu leo tunamaliza Bunge sasa tunaporudi kule tujue basi ni lini utatupa barabara hii mkandarasi alipwe *advance payment* ili aanze ujenzi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba useme neno Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara kama nimemsikia vizuri nadhani *Airport* - Kayenzi kwenda Nyanguge ni barabara ambazo tunasema ndio zinakwenda kupunguza misongamano katika miji yetu ikiwepo hiyo barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo tulishapata mkandarasi ambapo tulisema tutaanza kwa kilometa 10; ni moja ya miradi ambayo ilisimama ambayo tumesema sasa miradi yote iliyosimama ukiwepo huo mradi ndio tutaanza nayo na ndio kipaumbele chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge huo mradi pia unakwenda kutekelezwa kwa kuwa tumeshapitishiwa bajeti na Serikali imetoa maazimio hapa kwamba miradi yote iliyosimama itakwenda kuikamilisha ama kuijenga ile ambayo ilikuwa imesimama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. AMJADI USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa kuniona na kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ucheleweshaji sana wa malipo kwa wakandarasi hasa wakandarasi wa ndani, imekuwa wanachukua muda mrefu wengine hadi kufikia mwaka au miaka miwili, wamekuwa wakipata matatizo ya kufilisika na mikopo yao ambayo wanachukua benki na kiasi ambacho wengine wamekuwa hawafanyi kazi kwa ufanisi kama ambavyo wanafanya watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani sasa kuona inaweka mpango mahsusi wa wakandarasi hasa wazawa kuwa wanapata malipo yao kwa wakati ili na wao waweze kufanya kazi kama wanavyofanya makampuni mengine ya nje? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Pondeza kwa swali nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kama kuna jambo kubwa ambalo Bunge hili limelifanya lilikuwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba Serikali inaweka mipango madhubuti ya kuhakikisha kwamba wakandarasi wa ndani wanalipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, Serikali imetenga fedha ambayo itakuwa inalipa wakandarasi wote ambao walikuwa wanadai, lakini pia Bunge hili ndio limeielekeza Serikali na Serikali imekubali kwamba sasa ile fedha ambayo wakandarasi watakuwa wanafanya miradi itakuwa inakwenda moja kwa moja kwenye mifuko ya barabara ambapo sasa kutakuwa hakuna ucheleweshaji, fedha inaingia na fedha inatoka kwa ajili ya kulipa wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba tutaendelea kulipa yale madeni yaliyokuwepo, lakini wale wakandarasi watakaoanza sasa kufanya kazi hatutegemei tena kufanya kazi kwa mkopo kwa sababu tutakuwa na fedha ambazo sasa zinakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa Barabara. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea kuna tangazo la wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri ana dharura.

Wageni 28 wa Mheshimiwa Nhamanilo Reuben Kwagilwa, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni wapiga kura wake wa Jimbo la Handeni Mjini kutoka Mkoani Tanga. Ahsanteni sana na karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sasa namwita Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini aulize swali lake.

Na. 694

**Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi - Tarime**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatatua migogoro ya ardhi katika maeneo ya Korotambe na Remagwe, Marasibora Rorya na Nyamerambaro - Tarime?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Kaspar Kaspar Mmuya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii inahusu mipaka ya kiutawala. Mipaka ya Kijiji cha Korotambe na Remagwe iliwekwa mwaka 1996 na Serikali. Kijiji cha Korotambe kinatambua mpaka wao ni Mto Nyabichune kulingana na ramani za mipaka ya vijiji iliyoidhinishwa mwaka 2010 na kwa upande wa Kijiji cha Remagwe wao wanatambua mipaka yao ya asili ya mashamba iliyowekwa mwaka 1949 enzi za ukoloni wa Ujerumani ijulikanayo kama Ramani ya *DC Ingram*. Mipaka hii ya *DC Ingram* siyo inayotambuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kijiji cha Marasibora na Nyamerambaro mpaka wake ni sehemu iitwayo Mlima

Nyamerambaro. Wananchi wa vijiji hivi wote wanataka mipaka ya vijiji hivi iendane na mipaka ya mashamba yao kwa namna wanavyomiliki bila kuzingatia mpaka wa kiutawala uliopo baina ya vijiji hivi iliyowekwa na Serikali. Aidha, katika eneo hili la mipaka wapo wanavijiji wa Kijiji cha Marasibora ambao wako Rorya wanalima katika Kijiji cha Nyamerambaro ambacho kipo Tarime na wengine wapo Kijiji cha Nyamerambaro ambacho kiko Tarime, lakini wanaendesha shughuli zao za kilimo katika Kijiji cha Marasibora ambayo ni Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kusisitiza na kutoa elimu kwa wananchi wa vijiji hivi kuwa wanapaswa kuheshimu mipaka iliyowekwa na Serikali kwa mujibu wa *GN* za Serikali zilizoanzisha vijiji hivyo. Hata hivyo, Wizara ya Ardhi itashirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kushughulikia changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na kutuma timu ya wataalamu wa Wizara kwenda katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia majibu ya Serikali na naomba Bunge lijue kwamba eneo la Kurutambe na Remagwe na Marasibora na Nyamerambaro ni maeneo ambayo watu wameuana sana na wamejenga uhasama mkubwa na ndiyo maana ninaomba kwa heshima kubwa hao wataalamu waende. Pia, Mheshimiwa Waziri aende akawasikilize ili kuondoa changamoto ile ambayo na hata wakati wa siasa wako watu wanaenda kukaa upande huo kutuchonganisha kwamba hatuwatetei wananchi wetu. Hilo ndilo la kwanza lipewe uzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wakati naandika swali hili migogoro mingine miwili ya Bumera na Bunyama imeongezeka ambapo kuna mtu ana mfuko mkubwa wa pesa, anasumbua

wananchi, lakini eneo la Msege ya Ukoba kuna kigogo wa wilaya anachukua eneo la kijiji katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hali ilivyo kule Tarime Vijijini, ni lini Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri tutaenda katika maeneo yenye migogoro, badala ya kunisikia nikiongea kila siku, yeye awasikilize wananchi wangu ili wachukue hatua madhubuti kuondoa shida iliyopo Tarime Vijijini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Mwita kwa kuendelea kusisitiza jambo hili ili Serikali iweze kwenda kwenye eneo la tukio na kuweza kuwasikiliza wananchi hawa. Naendelea kukuahidi Mheshimiwa Mwita, Waziri wangu wa Ardhi ameshaongea tayari na Waziri wa TAMISEMI. Kwenye ratiba ya mwezi wa saba mwaka huu, katika maeneo ambayo yatatembelewa ni pamoja na maeneo ambayo umeyataja pamoja na kuongeza na migogoro hii miwili ambayo umeielezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie wewe pamoja na Wizara na pamoja na TAMISEMI tutakwenda kwenye maeneo haya na tutakamilisha migogoro hiyo na kuitatua moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Richard Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Njombe wamekuwa na mgogoro wa muda mrefu wa eneo la Mbarali. Kamati imefanya kazi kwa maana Kamati ya Mkoa wa Njombe na Kamati ya Mkoa wa Mbeya kubainisha maeneo ya mpaka kwenye

eneo la Mbarali na Makete, lakini Serikali hadi sasa hawajaweka *beacon* kwenye maeneo yale. Changamoto inayojitokeza ni nini Mheshimiwa Naibu Waziri, wananchi hawajajiandikisha kwa maana ya kupata *NIDA* kwa sababu hawajulikani wanatokea upande upi, lakini la pili, anwani ya makazi pia haijaweza kuwekwa kwa sababu hawaonekani wanaishi eneo gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipi kauli ya Serikali, mwende mkaweke *beacon* kwenye maeneo hayo ili kutofautisha wananchi wa Mbarali na Makete ili mgogoro huo uishe na wananchi waweze kupata huduma zingine stahiki za Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Mheshimiwa Sanga kwanza hongera sana kwa utulivu ambao unaendelea kuusisitiza katika maeneo haya ambayo umeyaeleza na ni kweli, ubainishaji wa mipaka hii tayari wizara ilishafanya na sasa hivi ilikuwa ni changamoto ya kwenda kuweka hizo *beacon*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nitumie hadhara hii na Bunge lako Tukufu kumwelekeza Katibu Mkuu, amwelekeze Mkurugenzi wa Ramani pamoja na Upimaji ili awaze kutuma wataalamu wake wakashirikiane pamoja na mikoa hii miwili pamoja na maeneo haya ya vijiji wakaweze kuweka *beacon* kulingana na mipaka ambayo imetambuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa halmashauri yetu ya Bagamoyo kumekuwa na ongezeko kubwa la migogoro ya ardhi, hususani maeneo ambayo yapo karibu na fukwe za bahari, ikiwemo Kata ya

Mapinga, maeneo ya Changwaela, na limezuka wimbi la wananchi kuja kusema kwamba hayo ni maeneo yao wakati wapo wananchi wamekaa zaidi ya miaka 20, 30 na wana hati zilizotolewa na mamlaka husika.

Je, Serikali haioni sasa ipo haja ya kuanzisha kliniki mahsusi ya ardhi ya kimkakati, kwa kuwa jimbo hili mmeliteuwa kuwa wenyeji wa mradi mkubwa wa viwanda ili kushughulikia migogoro hiyo ya ardhi, ili mwenye haki apate na kuleta amani katika Halmashauri ya Bagamoyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Bagamoyo, mara nyingi kwa kweli anaonekana kuelewa eneo ambalo analisimamia na katika kuwatetea wananchi kwa masuala mengi ambayo anaibua hapa bungeni, ikiwemo masuala haya ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Bagamoyo ni eneo ambalo tumelishughulikia kwa kiasi kikubwa sana katika kutambua migogoro yake, lakini pia kufanya kliniki nyingi katika maeneo haya kwa sababu ni maeneo ambayo yalikuwa yanavamiwa na watu wengi kwenda kuchukua ardhi kwa sababu ya fursa zilizopo za kiuchumi katika maeneo hayo.

Ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Pwani wanaendelea kila siku kushughulikia migogoro hii katika kila wiki kuwasikiliza na kuwatembelea. Juzi tu nimemuagiza Kamishna Msaidizi wa Mkoa wa Pwani kwenda katika maeneo hayo. Kwa sababu umeshaeleza *specifically* kata hii ambayo umeieleza, mimi ninaenda kuongea na Tume yetu ya Mipango ili iweze kuweka katika mipango yake ya kupanga vijiji, katika bajeti hii waone umuhimu wa kata hiyo ili waweze kutatua migogoro hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Thomas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Katavi ni jimbo ambalo lina migogoro mingi sana ya ardhi na bahati moja nzuri wakati Waziri Mkuu anafanya ziara, na wewe mwenyewe uliokuwepo na alitoa maelekezo na ulijionea hali ile, na hivi sasa Jimbo la Katavi kilimo kinaanza mwezi wa tisa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini sasa mmejipanga kwenda kutatua changamoto ya migogoro ya ardhi kati ya wananchi wa Jimbo la Katavi na misitu ya hifadhi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Thomas Kampala jambo hili ameshalileta kwenye Wizara yetu na mimi ninampongeza kwa sababu yuko pamoja na Wizara hii na sisi tumemwambia tutakwenda katika jimbo lake. Nimeshaweka katika ratiba baada ya Bunge hili, maeneo ambayo nitatembelea ni pamoja na jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Kampala, maelekezo ya Waziri Mkuu, sisi tumeshayapokea na tutakuja katika eneo hilo na tutaweza kuongea na wananchi na kutatua changamoto hizo, na Wizara pia ya Maliasili na Utalii pia itakuwepo katika msafara huo kwa ajili ya kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Arif Premji, swali la nyongeza.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Jimbo la Mtwara Vijijini, Kata ya Kitele, kuna uwekezaji wa kiwanda cha sukari; Kuna mgogoro mkubwa baina ya wananchi na mwekezaji huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kijiji cha Nakada na Lilido wameiomba Serikali ikiwezekana kupitia Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri aje kuwatembelea pale ili aweze kuwasikiliza changamoto hiyo na tuweze kupata ufumbuzi wa kudumu. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri anaweza kufika huko? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mbunge wa Mtwara Vijijini, kaka yangu na bahati nzuri ni eneo ambalo ndiko ambako Waziri wetu wa Ardhi anatokea kule na ameweka kwenye ratiba zake katika kipindi hiki baada ya Bunge atatembelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie, akinielekeza nitakuja haraka na kwa ratiba yake akija mwenyewe najua majibu yote yatapatikana katika muda ambao atakuwepo huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kijakazi Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. KIJAKAZI Y. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mgogoro wa ardhi kati ya Jimbo la Ruangwa ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri anatokea na Jimbo la Nachingwea katika eneo la Mbute, mgogoro umedumu kwa muda mrefu sana na ni kitendo ambacho kinasababisha

wananchi kushindwa kuendelea na shughuli zao za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kufahamu, ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wanatatua mgogoro huu ili shughuli ziweze kuendelea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Kijakazi Yunus, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Lindi, amekuwa karibu sana na majimbo yetu, mara nyingi anauliza kwa niaba yetu na anafuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, mgogoro huu naweza kusema siyo kama ni mgogoro, ni suala la kwenda kubainisha mipaka. Wananchi walioko kwenye Kijiji cha Mbute na vile ambavyo viko Ruangwa, ni suala tu la kuja kuwaambia mpaka wao uko hapa. Bahati nzuri amesema eneo hili lipo kwenye Jimbo la Ruangwa ambako mimi ndiyo mwakilishi wao. Nilishaenda kwenye eneo hili na nimeshaongea na Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa na Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, wataenda kwenye eneo hili kwa ajili ya kwenda kubainisha kwa sababu tayari wataalamu walishakwenda kutatua changamoto hii na tutakwenda kuweka mipaka ambapo tutaweka *beacon* kwa ajili ya kubainisha kabisa sasa mpaka ndiyo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi hiki ambacho nitakwenda jimboni, niwahakikishie vijiji hivi nitakwenda kwenye kata hizi na nitatembelea kwenye jambo hili na Mheshimiwa Fadhili Liwaka nimeshakubaliana naye, tutakwenda wote kwenye eneo hili kwenda kuongea na wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edibily Kinyoma, swali la nyongeza.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ni shahidi ulikuja jimboni kwangu ukajionea vijiji 27 vyenye mgogoro dhidi ya *TFS* na ukaahidi kwamba utarudi tena kuimaliza migogoro hii. Je, ni lini wewe na timu yako utarudi Jimboni Kasulu Vijijini ili kuhakikisha unaimaliza migogoro hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge wa Kasulu Vijijini ni kati ya Wabunge ambao ni wasikivu sana, lakini pia ni mtu ambaye anapenda amani. Amekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha wananchi ambao wanaishi kwenye msitu huo kuendelea kuwa na utulivu mpaka maelekezo ya Serikali ambapo yataletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nilimuahidi nitakuja kwenye maeneo hayo. Bado ahadi yangu iko pale pale na ninaendelea kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mkuu wa Wilaya ya Kasulu pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma kwa kazi kubwa wanayofanya katika kuwaambia na kuwaelekeza wananchi wanaoishi katika maeneo hayo, wafuate utaratibu na maelekezo ya Serikali ambayo yametolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kata ya Nyatwali natambua wananchi wamelipwa, lakini kuna baadhi ya maeneo matatu yalikuwa hayajafanyiwa tathmini na yamekuwa na mgogoro. Niishukuru Kamati ya Bunge ya Maliasili na Utalii iliwaita wananchi wangu pamoja wakawasikiliza na Mawaziri watatu; Waziri wa Fedha, wa Maliasili na Utalii pamoja na wa Ardhi. Wakakubaliana timu ya ardhi iende uwandani baada ya mwezi mmoja ilete majibu ya tathmini eneo la Magwata, eneo la Mjapani na eneo la *Irrigation System*. Mwezi umepita, wananchi hawana taarifa yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini sasa majibu kwa wananchi wa Nyatwali baada ya timu yenu kwenda uwandani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumpongeza dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, mara nyingi nilikuwa naongea naye na anasisitiza sana jambo hili la kupeleka taarifa ya tathmini ambayo Wizara yetu iliagizwa.

Naomba nimhakikishie, tutaileta tathmini hii kwa sababu ilikuwa maelekezo ya Kamati, tutaileta kwanza kwenye maandishi lakini pili, kwa sababu sisi tuna ratiba ya kwenda kwenye maeneo haya, tutakwenda kutoa taarifa hiyo kwa maelekezo ambayo tumepewa. Tutakwenda kutoa taarifa kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake.

Na. 695

**Kukutana na Wazazi wa Watoto Wanaoishi Mazingira Magumu**

**MHE. MABULA J. MAGANGILA** aliuliza:-

Je, upi mpango wa Serikali wa kuanza kukutana na wazazi wa watoto walio katika mazingira hatarishi ikiwemo watoto yatima na wenye ulemavu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfried Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuratibu vikao shirikishi vya kijamii vya kutoa elimu kwa wazazi na walezi kuhusu wajibu wao katika malezi, matunzo na ulinzi wa watoto hususan walio katika mazingira hatarishi wakiwemo watoto yatima na watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Mei, 2026, jumla ya wazazi na walezi 469,634 walifikiwa wakiwemo wanaume 178,343, wanawake 288,025. Kati yao, watu wenye ulemavu walikuwa 3,266.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu hii ni endelevu na inatolewa kupitia programu na kampeni mbalimbali ikiwemo Kampeni ya Familia Bora, Taifa Imara inayolenga kuimarisha malezi bora na ustawi wa watoto ndani ya familia na jamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, swali la nyongeza.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, miji yetu imejaa watoto wengi sana wanaoishi katika mazingira magumu na watoto hawa wametenganishwa na familia zao kwa sababu mbalimbali ikiwemo migogoro ya wazazi, wazazi kufariki na walioachiwa kushindwa kulea wale watoto.

Je, Serikali iko tayari kutoa mwongozo kwa wazazi wanaoishi na watoto wakiwaita watoto wa kambo, mwongozo upi ufuatwe ili watoto hao wasije kuwatelekeza?

Swali la pili, kwa kuwa Sheria ya Ulinzi wa Mtoto ipo na watoto hawa ni watoto wa Kitanzania, je, Serikali iko tayari kufungua kesi maalumu kwa ajili ya watoto wanaoishi mtaani ili waweze kupata haki yao kwa wazazi wao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza nipende kukupongeza sana Kaka yangu Mabula, kazi nzuri ambayo unaifanya kupitia hawa watoto ambao wanaishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mabula amekuwa akifanya kazi hii kabla hajawa Mbunge na anaendelea kuifanya. Ninampongeza sana na kadiri ambavyo tumeweza kuwasiliana mara kadhaa, kuona kwamba tunashirikiana kwa umoja wetu sisi kama Wizara, lakini na wewe pamoja na Wabunge wote na wazazi wengine wote kuona kwamba tunafanikisha kupunguza hawa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi bila sababu za msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tayari ina mwongozo kuona kwamba watoto hawa ambao wanaishi katika mazingira hatarishi wanaweza kupatiwa haki zao za msingi, lakini vilevile nipende tu kusema kwamba sheria ipo, Sheria ya Mtoto, Sura Namba 13 kifungu namba 51(b) inawataka wazazi kutimiza wajibu wao na walezi vilevile kutimiza wajibu wao na matunzo kwa watoto. Wazazi ambao wanakaidi kutimiza wao wajibu huo, wanakabiliana na faini zaidi ya shilingi 5,000,000, lakini vilevile wanaweza wakapewa kifungo si chini ya miezi sita na siyo zaidi ya miaka mitatu. Kwa hiyo, utaratibu huo upo na nipende kutoa wito kwa wazazi wote nchini, kila mzazi aweze kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugomvi ama umaskini si sababu ya kumwacha mtoto aende barabarani akalale kwenye *corridors*, apigwe na vumbi, apigwe na baridi, mvua, jua. Ni bora ukakaa na mtoto wako ukala naye ugali wa chumvi, ni bora ukakaa na mtoto wako ukanywa naye uji, ni bora ukalala naye njaa, kuliko kumwacha huyo mtoto apoteze haki zake za msingi.

Kwa hiyo, kama Wizara tutaendelea kusimama na kuhakikisha watoto hawa wanapata haki zao na wazazi wote ambao watakwepa jukumu lao la kutunza, kuwapa malezi na matunzo watoto hawa, sheria itafuata mkondo wake na kuanzia sasa tutakuwa wakali sana, hasa kwa wale ambao wanaingia kwenye migogoro ya mapenzi na kukimbia mimba, kukimbia watoto, kutelekeza wanawake na watoto. Tutawachukulia hatua kali sana na watu kadhaa tutawafanya wa mfano ili iwe komesho na karipio kali kuhakikisha watoto mtaani wanakwisha, wanabaki wakipata malezi kwenye familia, iwe kwa mzazi, kwa mlezi au ndugu wa wazazi.

**NAIBU SPIKA:** Naona Mheshimiwa Waziri amesimama.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa

*Engineer* Maryprisca Mahundi, nimeguswa na hoja hii na napenda niseme kwamba wazazi wote wa nchi hii ambao mmejaliwa matumbo yenu kubeba watoto mkawaleta duniani, mjue hiyo ni baraka. Pamoja na matatizo yote yanayoweza yakampata binadamu, akawa na hasira, asifikie wakati wa kumtelekeza mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ustawi wa Jamii tunapokea watoto wote ambao wanaonekana wana mazingira magumu kwenye kipindi fulani, kisha tunawatunza wasiende mtaani, tunarudi kwa wazazi tunaangalia kitu gani kinaendelea, tunarekebisha, wakipatana waje wamchukue mtoto wao. Kwa sababu bila hivyo akiingia mtaani, kwenda kumchukua ni gharama, lakini gharama kubwa inakuwa ameshabadilishwa akili yake na madhira mengi yameshampata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo niombe kupitia swali hili na majibu mazuri ya Naibu Waziri, wazazi, shida zote zikiwapata, mkavurugana, mtoto ni wa thamani kama dhahabu. Kama dhahabu usingeweza ukaiacha mtaani kisa umevurugana na mume wako/mke wako, ungeiweka mahali salama ukijua itakusaidia; Tuletee hiyo dhahabu ya mtoto, tumuweke mahali salama, akili zikiwarejea, mtachukua thamani yenu muendelee nayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shadya Omar, swali la nyongeza.

**MHE. SHADYA HAJI OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, napenda kwanza nipongeze Wizara hii kuwa na watu makini na kutupa matumaini kila uchao, majibu yenu yanatujenga na kutupa moyo kila uchao.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kanzidata ya kufuatilia watoto yatima pamoja na wenye ulemavu nchini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Shadya kwa kuwa *champion* wa kufuatilia masuala mazima ya watoto, mara zote amekuwa yuko mstari wa mbele kuhakikisha watoto wanabaki salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tayari kanzidata ipo, tuna mfumo jumuishi ambao unafuatilia watoto wenye mahitaji maalum, lakini vilevile katika mahitaji haya maalum tunaangalia watoto yatima na watu wenye ulemavu kwa sababu watoto hawa mtaani wao ndio wanaingia na kutoka mara zote, lakini ukitaka taarifa zaidi Mheshimiwa Shadya pamoja na wengine wote mnaweza mkaingia kwenye tovuti ya Wizara, uende ukaandike *Most Vulnerable Children Monitoring Information System,* pale utaona namna ambavyo Wizara tunafanya kazi kwa kina kuhakikisha kwamba tunatambua watoto ambao wana mahitaji maalum na tunawatendea haki kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mama mwenye upendo mkubwa, anatusisitiza kuhakikisha Taifa hili tunatengeneza Taifa la kesho imara kwa sababu hawa wa leo tusipowaangalia vizuri ndio ambao tutawarithisha. Kwa hiyo, tunawaangalia kwa karibu, kanzidata ipo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kuwa jamii yetu inatajwa mmomonyoko kuongezeka kila siku, na kwa kuwa ndani ya jamii yetu wapo wataalamu ambao ni wanasaikolojia wamekuwa wakifundisha jamii namna ya maadili kutokumomonyoka, je, ni upi mkakati wa Serikali

wa kufanya kazi kwa karibu na wanasaikolojia hawa ili kutengeneza mwongozo wa pamoja wa namna ya kufundisha, lakini ili kufaidika na maarifa yao. Nikimtaja mtu *specific* ambaye anafanya kazi nzuri *Aunt Sadaka Gandi,* ni namna gani mnashirikiana nao ili jamii iweze kunufaika kwa pamoja? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nampongeza sana *Engineer* Mwanaisha Ulenge kwa *commitment* yake ya msingi kabisa kuona kwamba mmomonyoko wa maadili ni jukumu letu sote. Kwa hiyo, ni lazima Serikali na watu binafsi tuweze kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ulenge naamini atakuwa na mimi akijua kwamba tayari tunafanya hivyo. Kama ulifuatilia kipindi cha *TBC* siku mbili hapa nyuma, *Aunt Sadaka* alikuwa pale *live*, lakini alikuwa na Mkurugenzi wetu Sebastian Kitiku, walifanya kazi nzuri sana ya uelimishaji. Hii ni endelevu na tunawaza siku moja tuwe na kongamano kubwa la mmomonyoko wa maadili la jumuishi. Waheshimiwa Wabunge tutawapatia taarifa, lakini baadaye baada ya Katibu Mkuu wetu Kaka Eliakim Maswi, kuweka vizuri mipango pamoja na Mkurugenzi Sebastian, hii itakuwa ni ya kwetu, kwa umoja wetu kuhakikisha kwamba tupige kelele, tuangalie zile mila na desturi nzuri ambazo zilikuza wazazi wetu hata sisi leo ni kizazi tunachoweza kurithishwa kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya unyago, masuala ya jandoni, yale salama ya kufundisha watoto nidhamu, mila na desturi nzuri nayo tutayajadili kwa umoja wetu. Tutakumbushana, tutarithisha kizazi hiki ambacho sasa ndio kinapotoka na kuona kwamba kwa umoja wetu tunakwenda kujenga jamii imara. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante na nashukuru na ninaamini nimejibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na utamaduni ambao unaendelea kukua kila siku, wazazi kutumia watoto wao ambao wengine walitakiwa kuwa shuleni, kwenda mtaani kwenda kuomba. Je, Serikali ina mpango gani au inatoa tamko gani dhidi ya watoto hawa ambao wanafanya kazi ambayo siyo ya kwao na kuacha masomo, matokeo yake wanashinda mtaani wakiomba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nipende kumpongeza sana Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kwa swali zuri.

Mheshimiwa Spika, kama unakumbuka nafikiri wiki iliyopita nimejibu swali linalofanana na hili, watoto wa mitaani wale wanaoombaomba, tunafanya kazi kubwa sana. Kwanza tutambue wale watoto wanaingia kutoka mikoa mbalimbali kupitia vyombo vyetu vya usafiri. Kwa hiyo, tumeweka madawati kwenye *stand* zetu kubwa zote na wilayani pia tunaendelea kuweka madawati. Kuona kwamba kwanza wale wanaoingia lile ingizo jipya tunawakamata pale ili wasiende kuongeza idadi kule mtaani. Maafisa Ustawi wetu wa Jamii wanafanya kazi nzuri, wanakaa nao, wanawauliza kwa upendo, watoto wanatoa ushirikiano. Mwisho wa siku, tunawarejesha kule walikotoka kwa msaada wa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuna watoto wengine siyo wa Kitanzania. Tunasema Tanzania ni nchi nzuri sana, watoto wanatoka nchi jirani, ukifika pale Mwanza watoto wanatoka nchi jirani, ukifika Mbeya watoto wanatoka nchi jirani, Dar es Salaam, Arusha hali kadhalika.

Kwa hiyo, pia wenzetu wa Uhamiaji tunafanya nao kazi kwa karibu sana, tukiwatambua tunaongea na balozi zao, tunawarejesha kule nyumbani. Nchi yetu kulingana na *green pasture,* hamna ambaye haipendi Tanzania. Tunawarejesha wanarudi, lakini tunaendelea kufanya kazi kuhakikisha kwamba wabaki kwenye nchi zao, waje huku kwa utaratibu na siyo kuzagaa mitaani.

Mheshimiwa Spika, lakini nipende kutoa wito kwa wazazi ama walezi, ama wanaojiita madalali, wanawachukua watoto mikoani wanawadanganya wazazi huko wanaenda kuwatafutia watoto ajira labda za ndani, wanaishia mitaani wanawatumikisha. Sheria itafuata mkondo wake na tutakuwa wakali sana na kuhakikisha kwamba hawa watoto wote wanatoka mitaani. Unaweza ukawa shahidi, wimbi lile la mwaka juzi siyo la leo, yote ni kazi nzuri inayofanywa na wenzetu wa Ustawi wa Jamii.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Regina.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, takwimu za sasa zinaonesha kuna ongezeko kubwa la watoto ambao wako mitaani na hii hali imekuwa ikijitokeza katika majiji makuu, lakini sasa tunaona ikijitokeza katika miji midogo.

Sasa nini kauli ya Serikali kuwa na mkakati wa kitaifa na wa haraka ili kuweza kunusuru hawa watoto waweze kurejeshwa katika familia zao na kupata haki zao na huduma za msingi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nipende kumpongeza sana Dkt. Regina kwa swali lako.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la watoto mitaani, mkakati wa kitaifa Mheshimiwa Regina ni kuhakikisha kwamba watoto hawa tunaendelea kuwachukua, tunaongea nao, lakini vilevile kuwarejesha kwenye familia zao. Kule kwenye familia ambazo bado zina migogoro, kuna mzazi mwingine hamtaki mtoto, kuna mtoto hamtaki mzazi. Hawa tunaendelea kufanya nao jitihada ya kuona kwamba wanapatana na ikibidi kutumia hata viongozi wetu wa dini. Mheshimiwa Mabula ameweza kufanya hilo.

Mheshimiwa Spika, pia, kutumia viongozi wa dini, mapadri, maaskofu, mashekhe kuongea na hawa watoto. Pia sisi kama jamii tusiangalie kama hiki ni kizazi ambacho kimeshindikana, ni watoto tu ambao wanahitaji upendo na kuongea nao kidogo.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa sisi sote viongozi, tufanye hili kwa umoja wetu, kwenye maeneo yetu, kule kama ni pembezoni mwa miji, chukua hawa watoto, ongea nao, kula nao taratibu, wapeni viongozi wa dini kulingana na imani ya mtoto. Utaona namna njema ya umoja wetu kufanikisha wimbi hili la watoto mitaani kwenda kukoma.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi.

Na. 696

**Kuongeza Ajira kwa Vijana katika Sekta ya Utalii**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza ajira kwa vijana na wanawake katika sekta ya utalii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuongeza ajira kwa vijana na wanawake katika sekta ya utalii nchini. Katika jitihada za kufikia malengo hayo, Wizara inaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji katika sekta ya utalii ili kuvutia wawekezaji zaidi na kuongeza fursa za ajira. Mathalani, mwaka 2017 Wizara ilifanya maboresho ya kanuni za usajili na utoaji leseni kwa kurekebisha takwa la idadi ya magari kwa Watanzania wanaotaka kufungua kampuni za kusafirisha watalii *(Tour Operators)* na kupunguza ada ya leseni, kupunguza gharama za malipo ya leseni za waongoza watalii, sambamba na kutoa mafunzo kwa waongoza watalii zaidi ya 2,200 nchini. Mikakati hiyo imewezesha Watanzania wengi ikiwemo vijana na wanawake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri sana, lakini pia ninaipongeza Serikali inapoendelea kufanya sensa ili kutambua idadi ya mamba wanaoleta madhara kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha vyuo vinavyotoa mafunzo ya utalii na ukarimu ili kuhakikisha ubora wa huduma hizo zinatolewa katika sekta ya utalii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali inakitumiaje Chuo cha Taifa cha Utalii ili kutoa mafunzo kwa vijana na wanawake wanaofanya kazi katika mnyororo wa sekta ya utalii? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Maryam Mwinyi kwa namna anavyofanya kazi zake kwa weledi na ufanisi mkubwa, lakini kwa kuwa miongoni mwa Wabunge ambao wanatetea vijana na wanawake kwa nguvu zake zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha vyuo hivyo kwa kuimarisha miundombinu mbalimbali ya kujifunzia na kujifundishia ili viweze kutoa mafunzo ambayo yanaendana na soko la ajira la kimataifa na nchini kwetu, lakini pia tunapitia mitaala mara kwa mara ili iweze kukabiliana na soko la ajira la kimataifa. Tunatumia vifaa vya kisasa na teknolojia ili kuwezesha vijana wetu na wanawake pia kuwa na taaluma ya kutosha kwenye kutoa huduma za utalii.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, hivi vyuo vyetu vinatoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa vijana na wanawake katika sehemu mbalimbali, kwa mfano, huduma za utalii, ukarimu, mapishi, kutoa huduma za chakula na vinywaji, uongozaji wa watalii, mapokezi na usimamizi wa huduma mbalimbali. Kwa hiyo, Serikali inaendelea siku zote kutoa mafunzo na kuwajengea uwezo vijana wetu wakiwemo hao wanawake. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Sasa tangazo la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu; Mheshimiwa Mussa Sima, Mbunge Mstaafu Jimbo la Singida Mjini. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Martin Lissu, mwanataaluma kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* na Ndugu Amani Kajuna, mfanyabiashara kutoka Jijini Mbeya. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Naibu Spika, wapiga kura wake kutoka Kijiji cha Minjingu, Mkoani Manyara, wakiongozwa na Mheshimiwa Stephen Mollel, Diwani wa Kata ya Nkaiti, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika Mstaafu ambaye ni Ndugu John Pepo, Afisa Utumishi wa Halmashauri ya Kinondoni, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni sita wa Katibu wa Bunge, marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam; Ndugu Ndebile Mashauri; Ndugu Tumaini Kamna; Ndugu Aloyce Lasway; Ndugu Harold Kayoza; na Ndugu David Kasira. *(Makofi)*

Wageni 18 wa Mheshimiwa Ayoub Mohammed Mahmoud, Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Zeyana Abdallah Hamid ambao ni viongozi wa Vyuo Vikuu na Kati kwa Mkoa wa Kaskazini, Zanzibar. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 48 wa Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, Naibu Waziri wa Ujenzi ambao wanafunzi wa kada ya uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM),* karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Johannes Lembulung' Lukumay ambaye ni Ndugu Riziki Yusuf Bendera, mpigakura kutoka Jijini Arusha. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Ndugu Willy Chaula, mfanyabiashara kutoka Makete, Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele ambao ni Mafrateli wa Seminari kutoka Jimbo la Morogoro. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Lucy Simirya Kombani ambao ni wanachama wa *Morogoro Secretary Sisterhood* kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, washindi wa wanawake vinara kutoka mikoa 12 ya Tanzania. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Ndugu Priscalis Lodrick na Ndugu Abraham Allen kutoka jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wanafunzi 90 na walimu 10 wa Shule ya Msingi na Sekondari *Al Hijra Islamic School* kutoka Wilaya ya Pangani, Mkoani Tanga. *(Makofi)*

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Nani, umesema kuna nini?

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mwongozo wa Spika.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Mwongozo.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie Kanuni ya 79 kuomba Mwongozo wako kwa kuwa Mkutano huu wa Tatu, pamoja na mambo mengine kupitia kiti chako ulitoa

maelekezo kadhaa kushughulikia suala zima la upatikanaji wa mafuta nchini na bei elekezi ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 Machi, mara baada ya tu ya Vita ya Iran, Marekani na Israel, kupitia mamlaka yako uliitisha kikao baina ya Wizara ya Nishati wakiwemo na Mawaziri wengine waandamizi na Kamati ya Nishati na Madini na ulitoa maelekezo mahsusi ya kuhakikisha kwamba Serikali inafanya kila jitihada ili nchi ipate mafuta wakati wote, pia kufuatilia mwenendo wa bei hiyo kutokana na athari ya vita iliyokuwa inaendelea.

Mheshimiwa Spika, tarehe 01 Aprili, mara baada ya *EWURA* kutangaza bei elekezi na kushuhudia kwa mara ya kwanza kiwango cha upandaji wa bei hizo kuwa kikubwa ulitoa maelekezo kwa Wizara ya Nishati kukutana na Kamati ya Nishati na Madini kushughulikia suala hilo na ikiwemo masuala ya upatikanaji wa uhakika wa mafuta wakati wote na bei zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Nishati ilifanya kazi hiyo, tulikutana na Serikali lakini pia kupitia wewe mwenyewe binafsi tulifanya vikao vya kimkakati vikihudhuriwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wengine kushughulikia suala hili la kadhia ya upatikanaji wa mafuta na bei yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo pia tumeendelea kushuhudia bei ikiendelea kupanda, lakini kabla ya Wizara ya Nishati haijawasilisha bajeti yake hapa ilifanya semina elekezi kwa Bunge zima na kwa Kamati ya Nishati juu ya hoja mbalimbali zilizohusiana na upatikanaji wa mafuta na bei zake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa tumeona duniani huko kwamba Iran na Marekani wamesaini makubaliano ya awali ya kusitisha vita na kuanza mazungumzo ya amani ambayo imeleta athari chanya ya kushuka kwa bei ya mafuta, kwa mfano inaonekana sasa bei ya mafuta kwa pipa moja mafuta ghafi ni dola 73.39 kutoka dola 100 mpaka 120 ya wakati ule vita inaanza.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba Mwongozo wako, je, Serikali inatuambia nini sasa kuhusu kushuka kwa bei ya mafuta duniani, tutarajie nini kwa bei za mafuta ndani ya nchi. Serikali inawaahidi nini wananchi kwamba lini tutarajie bei za mafuta zitashuka kutokana na athari chanya iliyopatikana baada ya kusitishwa kwa vita na kuingia makubaliano ya kuanza kwa mazungumzo ya amani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

Waziri wa Nishati upo, hebu tupe maelezo. Huo ndiyo Mwongozo wangu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwa mara baada ya vita kati ya Iran, Israel na Marekani kuanza tarehe 28 Februari, 2026, tulipata changamoto ya kufungwa kwa Mlango wa Hormuz ambao mlango ule unapitisha 20% ya mafuta ghafi ya dunia nzima, lakini si tu 20% kwenye mafuta ghafi, mafuta ambayo ni *refined,* mlango ule unapitisha karibia 34%.

Mheshimiwa Spika, wiki ya kwanza ya vita ile, tuliona *refinery* ya Ruwais inayomilikiwa na kampuni ya mafuta ya *Adnoc* ilipigwa, na baadaye *refinery* inayomilikiwa na kampuni ya *Aramco* iliyopo Fujairah nayo ilipigwa, ambayo ilipelekea kuleta upungufu mkubwa sana wa upatikanaji wa nishati ya mafuta duniani kote na ilipelekea pia bei za mafuta kuanza kupanda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona athari hizo, Serikali ilimtaka *EWURA, PBPA* (Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja) kwa kushirikiana pia na *TPDC* kuweza kukaa na kuangalia bei za mafuta na mwenendo wake duniani. Baada ya kuona hivyo, walichukua hatua za haraka za kuhakikisha kwamba tunapata kwanza *security of supply,* uhakika wa upatikanaji wa mafuta katika Taifa letu. Na

wewe ni shahidi na Bunge lako ni shahidi, katika kipindi chote cha mgogoro wa Mashariki ya Kati, Taifa letu halijakumbwa na uhaba wa mafuta. Ulikuwa ukitoka Dar es Salaam mpaka Kyerwa, mafuta yapo katika vituo vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bei ambazo zilikuwa zimepatikana katika kipindi cha vita cha mwezi wa tatu katika *region* yetu hii ya Afrika Mashariki, ndiyo ilikuwa bei ndogo kuliko wengine hadi kupelekea nchi nyingine kutaka kuja kuchukua mafuta kwetu. Hata katika bei za mwisho kwa mlaji, soko la Tanzania, wote ni mashahidi na vyombo vya habari mmekuwa mkiona vikitoa, bei yetu katika pampu imeendelea kuwa bei ndogo kuliko nchi nyingine zinazotuzunguka katika ukanda wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya Serikali kupitia *TPDC, EWURA* na *PBPA* kufanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba hatupati uhaba wa mafuta wakati wa vita.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba sasa baada ya mazungumzo yale ya amani kufanyika na kupatikana kwa *ceasefire* ya siku 60, bei ya soko la dunia ya mafuta ghafi imeanza kushuka na sasa imefika mpaka dola 70 kwa *barrel*. Serikali imewataka *TPDC, PBPA* na *EWURA* kuhakikisha ya kwamba Mtanzania naye anaanza kuona bei ile ikishuka katika vituo vyetu vya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Watanzania wataanza kuona bei ya mafuta ikishuka na kadiri mzigo unavyozidi kuja wa bei nafuu, kwa sababu kwa sasa kuna meli ambazo ziko njiani, kuna meli zilizofika bandarini, kuna mafuta yaliyoshushwa, yaliyokuwepo katika *storage*. Kadiri meli zinavyoanza kuja, zinazotoka za mzigo wa bei nafuu na bei zitazidi kushuka. Na tunatarajia, hata wataalamu duniani wametoa takwimu, tunatarajia kwamba ndani ya wiki nane mpaka wiki kumi dunia itarejea katika bei zilizokuwepo Februari, 2026.

Mheshimiwa Spika, katika soko letu Tanzania, tumewataka *EWURA* kuhakikisha Mtanzania anaanza kuona punguzo la bei hiyo kuanzia mwezi huu unaokuja kwenye bei ambazo zitatangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuangalia hali ya Mashariki ya Kati inavyoendelea, kwa sababu mafuta yetu tunaagiza kwa 100% na katika 100% ya mafuta tunayoyaagiza Tanzania, 61% yanatoka Mashariki ya Kati ambayo yanapita katika Mlango wa Hormuz, na 40% tunapata kutoka nchini India. Tutaendelea kuona ni namna gani tuna-*diversify* upatikanaji wa mafuta katika Taifa letu,

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa maelekezo yake Mheshimiwa Rais wetu, tunaangalia ni namna gani sasa tutapata *refinery* yetu pale Tanga ili tuweze kuweza kusafisha mafuta yetu wenyewe na sisi tupo katika eneo zuri katika bara letu, na katika nchi zenye miundombinu ya mabomba ya mafuta, Tanzania katika ukanda wetu inaweza ikawa ni namba moja. Tuna bomba la *TAZAMA* linalotoa mafuta Dar es Salaam bandarini kuelekea Ndola, lakini vilevile tuna *crude pipe* ambayo inatoka Uganda kuja Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna mpango wa kuweza kuwa na bomba la mafuta ambalo litachukua mafuta Tanga kupitisha kwenye baadhi ya mikoa yetu na kupeleka nchini Uganda.

Kwa hiyo, kuwa na *refinery* hapa katika Mji wetu wa Tanga, tutaweka mabomba kutoka Tanga - *TAZAMA* ili mafuta yanayoenda nchi za *SADC* yaweze kupita humo na yale ambayo yanaenda Uganda. Kwa hiyo, tuna mipango mikubwa ya kuhakikisha kwamba haya hayajitokezi tena ya kuweza kupata hitilafu au changamoto ya bei katika nchi yetu pale ambapo kutatokea migogoro huko duniani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa taarifa hiyo, nikuhakikishie kwamba mafuta Tanzania yataendelea kupatikana kwa uhakika na bei zitaanza kushuka mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Kuna Mwongozo mwingine, nani huyo. Ado, siyo wewe?

Nimesikia sauti kama inatoka huku. Haya Mheshimiwa Chinyele.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. PASCAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Spika, ninasimama kwa Kanuni namba 79, lakini pia ninasimama kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na taharuki katika mitandao mbalimbali ya kijamii kuhusiana na maandamano ambayo yanasemwa kupangwa na watu wasiyofahamika hapa nchini. Taharuki hiyo inaonekana kuwakumba hata watu katika mitaa na vijiji mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, je, suala hili Serikali inalifahamu na iwapo Serikali inalifahamu suala hili, je, inachukua hatua gani ili kuwahakikishia Watanzania usalama wao pamoja na mali zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani yupo? Waziri wa Mambo ya Ndani, Mwongozo nakupa wewe.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ambayo umenipatia kujibu au kutoa hoja ya Serikali juu ya Mwongozo ambao umeombwa na Mheshimiwa Pascal Chinyele.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mpaka sasa nchi yetu iko salama, hali ya nchi yetu ni tulivu na amani ipo kila mahali, isipokuwa zipo taarifa mbalimbali ambazo zinaenezwa kwenye mitandao ya kijamii, wapo baadhi ya watu wanatumia vibaya mitandao ya kijamii na kuzua taharuki. Wapo wanaosema kutakuwa na maandamano na maandamano yenyewe sababu hazitajwi, lakini hata wale ambao wamejaribu kutaja sababu ni zile ambazo Serikali imekwishatolea suluhisho, mojawapo likiwa la Katiba Mpya, ipo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na hatua mbalimbali zimekwishakupangwa za Kiserikali katika namna ya kuliendea jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, yapo maelezo mengine ambayo kimsingi yamekuwa ni ya kichochezi tu, yanafanywa na watu mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii. Sasa hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kuwa salama, moja ya hatua ambazo tumeendelea kuzichukua ni kwamba jambo la ulinzi na usalama wa nchi yetu dhamana hiyo tumepewa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mujibu wa Katiba, ku-*maintain order, peace and tranquility.* Kuhakikisha kuna amani, utulivu na utii wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jukumu hili ambalo tumepewa tumekwishaanza kufuatilia viashiria vyovyote vya uvunjifu wa amani kwa yeyote ambaye anapanga kuvuruga amani ya nchi hii kupitia mitandao ya kijamii au moja kwa moja katika jamii yetu. Tumeanza kufanya na kuchukua hatua juu ya maeneo ambayo yamepelekea kuleta matishio ya amani. Moja ya maeneo hayo yamekuwa tukiyashuhudia kwenye mikusanyiko mbalimbali ya watu ambao wamekuwa wakitoa taarifa zinazohusiana na kuvunja amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Tanzania siku tatu zilizopita lilitoa tamko la juu ya hali ya usalama kuwa ni shwari, lakini lilitahadharisha watu ambao wamekusudia kufanya uhalifu wa kupanga au kuandaa maandamano yasiyoruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia nafasi hii; moja niwaelekeze na kumuagiza *IGP* Camilius Wambura, atoe maelekezo kwa ma-*RPC* wote nchini katika mikoa ambayo yatashuka kwa Wakuu wa Polisi Wilaya mpaka kwenye Polisi Kata kuanza kufanya uratibu wa mipango ya kiusalama ambayo tunayo, lakini kuimarisha zaidi, mipango ya kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama katika kila eneo kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji mpaka kwenye kata na mitaa katika kipindi chote cha nchi yetu katika shughuli mbalimbali ambazo pia zinakusudiwa kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tunatarijia kuwa na ugeni mkubwa katika Maonesho ya Sabasaba, ambapo tunatarajia kupata wageni kutoka nchi mbalimbali. Katika kipindi hiki ndicho ambacho kinatusaidia kujijumuisha katika kujenga uchumi wa nchi yetu. Sasa katika kipindi hiki ambapo kuna chokochoko hizi hatutaweza kumvumilia mtu yeyote kimsingi ambaye atafanya vurugu za aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni katika kipindi ambacho tunatarajia shughuli zote za kiuchumi ziendelee na ninawahakikishia wakulima kama ni shambani waendelee kwenda kufanya shughuli za kilimo; wafanyabiashara waendelee kwenda kufanya shughuli za kibiashara; wasafirishaji waendelee na shughuli za usafirishaji, watumishi wa Serikali na watumishi kwenye maeneo mbalimbali waendelee kwa sababu tumejipanga vizuri kuhakikisha tunadhibiti uhalifu wa aina yoyote ambao utafanywa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kama kuna hoja za msingi kwa sababu mpaka sasa Serikali haijapata hoja yoyote ya msingi ya kwa nini watu waende kufanya vurugu au kuandamana. Kama hoja

yoyote ya msingi ipo, mimi nitasimama kwa niaba ya Serikali, nitazipokea hoja hizo zifikishwe kwa Waziri wa Mambo ya Ndani na popote kwenye mamlaka ya nchi ambapo zitahitajika kufika, tutazifikisha huko, lakini mpaka sasa tunavyozungumza hakuna hoja yoyote ya msingi ambayo imeelezwa kwamba Serikali imeshindwa kuitolea majibu au kuchukua hatua.

Kwa hiyo, bado pia katika masuala ya taarifa ambazo zimekuwa zikitokea kwenye masuala ya uhalifu, tutaanza kuanzia kesho kuwahoji watu mbalimbali ambao wamekuwa waziwazi na ushahidi na vielelezo wakichochea uvunjaji wa amani katika Taifa letu, kufanya vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazo *clip* za *video* ambazo wamezungumza kwenye *platform* mbalimbali za mitandao. Tunao ushahidi ambao tumeukusanya wa watu *(primary evidence)* au *eye witness* na wale waliosikia, zipo na tuna huo ushahidi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia kesho namuagiza *IGP* Wambura, tuanze kuwaita hao watu na kuwahoji na wale ambao vielelezo na ushahidi wao uko dhahiri, tutawafikisha mahakamani. Kwa hiyo, hatutamfumbia macho mtu wa aina yeyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo wengine ambao wanafadhili uhalifu, hatuko tayari kurudi tena kwenye mambo ambayo yametweza na kuharibu rasilimali za nchi yetu, hatuwezi kuruhusu watu wetu waumizwe, hatuwezi kuruhusu biashara zisimame, hatuwezi kuruhusu shughuli za kiuchumi zisimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili na kupitia Bunge lako Tukufu nakuhakikishia kama itatokea kuna mtu ambaye anadhani yeye yuko juu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 30 kwamba atavunja na haki yake ni ya msingi kuliko haki za wengine, huyo tutahitaji kumfikisha mbele ya mahakama akajibu mashtaka hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kuna mtu anadhani hana wajibu ambao umetajwa kwenye Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wajibu wa kila mwananchi kuilinda nchi yake, kulinda usalama wa wengine, mali za wengine na kulinda Taifa lake, ntu yeyote pia asiyetimiza wajibu kwa sababu kwenye sheria *act or missiyon;* kwa mtu atakayetenda au atakayeacha kutenda kuzuia tendo la uhalifu, nao pia hao ninakuhakikishia tutachukua sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwakumbishe na kutoa rai kwamba tunayo Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi hii inaongozwa kwa mujibu wa Katiba, nchi hii ni ya kidemokrasia na inayofuata misingi ya utawala wa sheria, haki za binadamu na inaheshimu misingi yote ya utawala bora. Kwa sababu tunayo Katiba ya Watanzania wote na kwa sababu tunayo Sheria ya Kanuni za Adhabu inayohusika kwa Watanzania wote bila kujali ni tajiri au maskini, bila kujali hali au mahali anapotoka, bila kujali hadhi au heshima hata kama uwe na nafasi, huna nafasi, unawajibika kufuata na kutii sheria. Kwa hiyo, hatutavumilia kwa yeyote yule ambaye atavunja sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia kwa sababu ya taharuki hizi ambazo zimekuwa zikiendelea, ninatumia fursa hii pia kwa sababu tumekuwa tukisikia majibizano ya hapa na pale, kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo ni *custodian* wa *peace, order and tranquility,* kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo tumepewa *instrument* na dhamana ya kusimamia amani, ulinzi na usalama, na kwa sababu uchochezi wa mambo haya umeonekana zaidi kwenye maeneo ya kisiasa, kupitia Bunge lako Tukufu namuelekeza *IGP* Wambura asitoe vibali kwa kazi zozote zitakazokuwa zinahusiana na kufanya mikutano ya hadhari katika kipindi hiki kwa chama chochote, iwe Chama Cha Mapinduzi, iwe chama chochote kile kwa kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri turudi katika kuwaruhusu wananchi wajenge uchumi wa nchi yao. Ni katika kipindi ambacho tunahitaji

kufanya kazi kwa ajili ya kuhakikisha kila Mtanzania, wafanyabiashara, wawekezaji wanafanya kazi yao kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafanya hivi kwa sababu katika mazingira haya tutakapokuwa tunawatafuta wahalifu ni ngumu kuchambua wahalifu kwenye mkusanyiko wa watu wengi, kwa hiyo, ni vizuri tujue hata kama hali itaendelea kuwa na matishio haya, kwa sababu wapo ambao wametishia na tumewakamata wengine, wana madumu ya petroli, tumewakamata wengine wana silaha, tumewakamata wengine wapo ambao wanapanga mikakati ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, tukienda kwa hatua hii, tumeendelea kuzuia hata pale Dar es Salaam, Oysterbay na Masaki, baa ambazo hazijafuata utaratibu tunazizuia kwa kipindi hiki zisifanye kazi kwa kufuata Sheria ya Mazingira ambayo sisi pia ni *custodian* wa kusimamia *enforcement* ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo yote katika kipindi cha usiku ambao yana matishio ya usalama, uchunguzi ukifanyika na ikaonekana kuna *tensiyon* za kiusalama, naagiza kupitia Jeshi la Polisi, *IGP* Wambura na ma-*RPC* wote na Kamati za Usalama, msisite kuwafungia katika kipindi hiki kwa sababu tunahitaji amani na utulivu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika eneo lingine kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa ya Wakuu wa Wilaya kwa sababu wanabeba dhamana ya kuwa Wakuu wa Kamati za Ulinzi na Usalama, niombe sana, lakini pia niwaagize kupitia nafasi ya Amiri Jeshi Mkuu, ambao wao wanafanya kazi chini yake, kuhakikisha kuna amani na utulivu kwenye maeneo yao. Waanze sasa kutengeneza zile timu na wanajua namna ya kuratibu, mengine hatutayasema hapa, lakini wanajua uratibu na utaratibu wa siri wa kutafuta wahalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitumie fursa hii, wamiliki wa hoteli zote, *Air B&B, guest houses* na *lodge* nchini kuanza kusajili kila anayeingia mle ndani kwa kutumia vitambulisho vya *NIDA*. Wageni wote wanaoingia kwenye majiji, miji, wajisajili, anapoenda kwenye hoteli yako au *lodge* tukakuta kuna watu wameingia na hawana vitambulisho, hawaeleweki walipotoka, tutachukua hatua dhidi ya mmiliki pamoja na muhudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mengine ambayo ni ya ndani sana ya kimedani siwezi kuyazungumza kwenye hatua hii, lakini kwa sasa itoshe kusema nchi yetu ipo salama, tutaendelea kuilinda, amani na utulivu utaendelea kutamalaki katika Taifa letu na hakuna mtu mwingine yeyote kwa mujibu wa sheria tulizonazo atatupangia namna ya kusimamia usalama wa nchi yetu, Taifa letu na rasilimali za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusemahayo naomba nikushukuru sana, sisi tukitoka hapa tunaenda kufanya kazi hii ili kuhakikisha Watanzania wanakuwa salama, mali zao zinakuwa salama na uwekezaji wa Taifa letu unakuwa salama, wawekezaji wanakuwa salama na *vital installation* zote maeneo muhimu ya utoaji wa huduma za jamii yanakuwa salama. Hakuna hospitali itafungwa, hakuna soko litafungwa, hakuna kibanda chochote cha biashara kitafungwa, watu watakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho ya Sheria Mbalimbali zipatazo saba kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamebainika wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo *(A Bill for An Act to amend certain written laws in order to keep the Laws updated with some challenges observed in its implementation)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Muswada huo ninaupeleka kwenye Kamati ya Katiba na Sheria.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Kilimo kwa lengo la kuboresha kanuni, usimamizi na maendeleo ya sekta ya kilimo pamoja na masuala mengine yanayohusiana na hayo *(A Bill for An Act to amend certain agricultural laws with a view to improving the regulation, administration and development of agricultural sector and related matters)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Muswada huo ninaupeleka kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto na kuweka masharti kuhusu uhamisho wa mali, madeni pamoja na watumishi wa Bodi ya Pareto, kuweka masharti ya mpito na masuala mengine yanayohusiana na hayo.**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Muswada huo nao vilevile unakwenda kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025 naomba kutoa taarifa kuwa shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Tatu wa Bunge sasa zimemalizika.

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyosikia shughuli zote zimekamilika, sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu aje atoe taarifa yake. Karibu Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa fadhili zake zilizotuwezesha sote kuiona siku hii muhimu katika historia ya Bunge la Kumi la Tatu.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu tumekutana leo kwa ajili ya kuhitimisha Mkutano wa Tatu ambao ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kupokea na kujadili bajeti ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nimesema leo ni siku muhimu na ni ya kihistoria kwa sababu hii ni bajeti ya kwanza kupitishwa na Bunge la Kumi na Tatu baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025, hongereni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa naomba nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono na uongozi wake thabiti wakati wote wa kipindi cha Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Bajeti, wakati wote amekuwa akinipa maelekezo yenye tija na kuifanya kazi yangu iwe nyepesi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri pamoja na michango ya Wabunge katika Bunge hili yalitoa mwelekeo sahihi katika mipango na utendaji wa shughuli za Serikali na imegusa moja kwa moja maisha ya Watanzania wote.

Pia, niwapongeze kwa kazi kubwa mliyoifanya tarehe 23 Juni, 2026 ya kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali kwa kura ya ndiyo kwa bajeti ya 2026/2027 bajeti ya shilingi trilioni 62.33 kwa kura za 97.66%; hongereni sana Waheshimiwa Wabunge na hiyo kazi mliyoifanya inaashiria imani mliyoayo kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga, imesikiliza hoja zenu na kutoa ufafanuzi na sasa ipo tayari kutekeleza bajeti kwa kuzingatia yale yote Waheshimiwa Wabunge mliyoyasema.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala, Naibu Makatibu Wakuu,

Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali, watumishi wote wa umma kwa kufanikisha kupitishwa kwa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo utakumbuka, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Emmanuela Se-Mtatifikolo, Mbunge wa Jimbo la Isimani kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa jimbo hilo kufuatia uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushindi huo unadhihirisha kwamba wananchi wa Jimbo la Isimani wana imani kubwa na Chama Cha Mapinduzi kutokana na uongozi thabiti, sera makini pamoja na ilani ya uchaguzi inayotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumkaribisha sana Mheshimiwa Emmanuela Se-Mtatifikolo na nimhakikishie kuwa Waheshimiwa Wabunge wote na Serikali tutampa ushirikiano mkubwa ili aweze kutekeleza majukumu kikamilifu ya kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Isimani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Mkutano wa Tatu wa Bunge ukiendelea, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya teuzi mbalimbali. Teuzi hizo zilifanywa kwa lengo la kutekeleza na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi na shughuli mbalimbali za Serikali. Moja, mnamo tarehe tarehe 02 Mei, 2026 Mheshimiwa Rais alimteua Mheshimiwa Dkt. Evaline Wilbard Munisi, Mbunge kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Mahusiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, Mheshimiwa Rais alimteua Dkt. John Antony Jingu kuwa Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, aliteua wakuu wa taasisi, mabalozi na wateule wengine katika nafasi mbalimbali. Nitumie fursa hii

kuwatakia wateule wote kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao mapya na kuwakumbusha wajibu wao wa kutanguliza masilahi ya Taifa letu mbele na kuwahudumia Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kutoa pole kwa Watanzania wenzetu waliokumbwa na majanga mbalimbali zikiwemo ajali za barabarani na ajali zinginezo. Ninatoa pole kwa wananchi wote waliopoteza wapendwa wao katika ajali hizo na vilevile natoa pole kwa majeruhi wote na ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka majeruhi wote. Nitumie fursa hii pia kutoa pole kwa waathirika wa majanga mengine yote ambayo yalitokea.

Mheshimiwa Spika, leo wakati tunahitimisha shughuli za Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu tumefanikiwa kutekeleza masuala mbalimbali ikiwemo wajibu wa msingi wa kutunga sheria, kupitisha bajeti, kujibu maswali na hoja zilizojitokeza. Kwa upande wa hoja zilizojitokeza tumejadili na kupitisha iswada na sheria mbalimbali, kujadili na kutoa maazimio mbalimbali na kiupekee katika mkutano huu maswali ya msingi yaliyojibiwa ni maswali 689 na maswali ya nyongeza yaliyojibiwa ni maswali 2,608 na maswali 27 ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu yaliulizwa na kupatiwa majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miswada katika mkutano huu Bunge lako Tukufu limepokea miswada mitano ambayo ilisomwa kwa hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2026 ulisomwa kwa hatua zote;

(ii) Muswada wa Sheria ya Matumizi wa Mwaka 2026 ulisomwa kwa hatua zote;

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 02 wa Mwaka 2026 ulisomwa kwa mara ya kwanza;

(iv) Mswada wa Sheria Marekebisho ya Sheria za Kilimo 2026 nao ulisomwa kwa mara ya kwanza; na

(v) Muswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 nao ulisomwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 61 na 107 hadi 112 za Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari 2023 na kwa kuzingatia wajibu wa Bunge; Bunge lako Tukufu lilipokea na kujadili azimio moja ambalo ni Azimio la Bunge kuhusu Kuipongeza Timu ya Taifa ya Vijana Wanaume chini ya umri wa miaka 17 yaani *Serengati Boys* kwa kufuzu fainali za *AFCON 2026* na kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia la Vijana Chini ya Umri wa miaka 17 kwa mwaka 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirejee kuwapongeza sana vijana wetu hawa kwa kuweka historia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake thabiti na dhamira yake ya kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kwa weledi mkubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Dhamira hiyo imekuwa msingi wa mafanikio makubwa tunayoshuhudia katika mwaka wa fedha ambao tunahitimisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maono na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya Awamu ya Sita imepata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2020 na Dira 2025 kupitia sekta mbalimbali. Mafanikio haya yamebainishwa kwa kina wakati nilipowasilisha Bungeni mapitio ya Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu mapitio pamoja na uelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, pia, mafanikio hayo yamebainishwa katika maeneo ya miundombinu, sekta za uzalishaji, huduma za jamii na masuala mtambuka na yamebainishwa kwa ufasaha na Waheshimiwa Mawaziri wa kisekta kupitia bajeti za Wizara zao katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026. Mafanikio kwenye sekta na maeneo hayo yameendelea kuwa faraja na ukombozi kwa wananchi wa kipato cha chini ikiwemo wakulima, wafanyabiashara wadogo, waendesha bodaboda, mama lishe na baba lishe na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, haya yote ni matunda ya uongozi makini wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na dhamira yake ya dhati ya kustawisha maisha ya Watanzania na kuwa na kazi za staha na utu bila kuacha mtu yeyote nyuma.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kujivunia kuona jinsi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyoendelea kuitangaza na kuiwakilisha vyema Tanzania katika jukwaa la kimataifa. Mheshimiwa Rais ameendelea kuonyesha uongozi na hekima na kuendelea kushirikiana na mataifa mbalimbali na asasi za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameendelea kusukuma mbele ajenda ya diplomasia ya kiuchumi kwa vitendo na kuudhibitisha kuwa Tanzania ni mshirika mkubwa na wa kuaminika katika biashara na uwekezaji. Tumeshuhudia ziara za viongozi wenzake kutoka Mataifa ya Ghana, Kenya, Uganda, Rwanda, Singapore na hivi majuzi kiongozi kutoka Namibia.

Mheshimiwa Spika, ziara hizo zinafanikisha makubaliano pamoja na kusaini mikataba muhimu katika maeneo ya biashara, uchukuzi, nishati pamoja na miundombinu. Aidha, Mheshimiwa Rais alipokea hati za utambulisho kutoka kwa mabalozi wanane akisisitiza umuhimu wa nchi za Afrika kuongeza thamani za rasilimali zake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais pia ameitangaza Tanzania kama Kituo cha Uwekezaji wa Kimataifa kupitia ziara zake

za kikazi nje ya nchi akiwa amefanya ziara akishiriki mikutano ya kikazi na ya Kiserikali katika nchi za Falme za Kiarabu na Urusi.

Mheshimiwa Spika, akiwa nchini Urusi Mheshimiwa Rais alitoa wito wa uwekezaji zaidi katika Bara la Afrika akiitangaza Tanzania kama lango la kimkakati la biashara katika eneo lenye soko la zaidi ya watu milioni 500.

Mheshimiwa Spika, ni heshima kubwa pia kwa Taifa letu kuona Mheshimiwa Rais akitunukiwa Shahada ya Heshima ya Uzamivu wa Chuo Kikuu cha Urafiki wa Watu wa Urusi kwa mchango wake mkubwa katika elimu, ushirikiano wa kimataifa na urafiki katika mataifa haya. Heshima hii iliyotolewa hutolewa kwa nadra kwa viongozi wachache duniani na hii ni kielelezo cha namna jamii ya Kimataifa inavyodhamini uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunampongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa heshima hiyo aliyotuingizia sote kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi wa Tanzania kwa ujumla kwamba vipaombele vya bajeti ya 2026/2027 kwa kila Wizara za Kisekta vimezingatia masilahi mapana ya Taifa. Bajeti hii inaendelea kuimarisha uwekezaji katika sekta za uzalishaji, miundombinu na huduma za jamii. Serikali imejipanga kuendelea kuimarisha mikakati na mifumo ya kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa mikopo na misaada kutoka nje mikakati mojawapo ni pamoja na kudhibiti matumizi ya umma katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla wameshuhudia kusomwa kwa bajeti ya mwaka 2026/2027 na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji ambao waliwasilisha bajeti pamoja na mpango wa Taifa. Bajeti hiyo inaenda kugusa na kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ambayo inaajiri vijana na Wanawake wa Kitanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa inaenda kutenga 15% ya mapato yao ya ndani badala ya 10% iliyopo kwa sasa ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu na kati ya 15% iliyotengwa 10% inaelekezwa kwenye mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kama ambavyo uwiano ulikuwa awali.

Mheshimiwa Spika, aidha 5% itatumika kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya ujenzi wa maboresho ya masoko na maeneo ya biashara na ujasirimali ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira hususan kwa vijana, wanawake na makundi maalumu.

Mheshimiwa Spika, nizielekeze Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo ya wajasiriamali kwa kuzingatia urahisi wa kufikika na kuwawezesha kufanya biashara kwa tija.

Mheshimiwa Spika, hivyo kupitia 5% ya uboreshaji wa miundombinu ya wajasirimali ya mali pale itakapohitajika na halmashauri zilipe fidia wasisite kufanya hivyo ili kuwezesha upatikanaji wa maeneo yenye sifa kwa wajasirimali kupata tija zaidi ili tuache kufukuzana fukuzana na wajasiriamali pale tunapowapatia eneo ambalo halifikiki au ambalo halikidhi mahitaji ya biashara wanazozifanya. Tuwapatie maeneo ya kufanyia biashara katika mazingira yanayokidhi mahitaji ya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia utaratibu mpya wa utoaji wa mikopo inayotokana na 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri ninazielekeza taasisi za fedha na waratibu wa mikopo hiyo kuondoa masharti magumu yanayokwamisha wajasiriamali kunufaika na mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano ulazima wa wahitaji kwa upande wa watu wenye ulemavu kuunda vikundi na ulazima wahitaji kuwasilisha dhamana kubwa kama vile hati za nyumba, hati

za vitu vingine vikubwa ambavyo kwa asili ya biashara zao hawawezi kuwa nazo.

Mheshimiwa Spika, kipekee ninatoa wito kwa vijana kujipanga na kutumia ipasavyo vipaji walivyonavyo, fursa zilizopo na mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali katika kujiongezea kipato kupitia shughuli wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, zamani ilikuwa hata watu wenye ulemavu lazima wawe na kikundi, tunaondoa sharti hilo ili kuwawezesha kufikia mikopo hiyo bila kulazimika kuunda vikundi kadhalika kuondoa masharti ya hati za nyumba kwa bodaboda, mama lishe na watu wenye ulemavu pale wanapohitaji mikopo hiyo. Watumie Vitambulisho vya Taifa kupata mikopo hiyo kama dhamana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuwavutia wajasiriamali, Serikali inatoa msamaha wa kodi ya mapato kwa wafanyabiashara wadogo ambao ni wapya kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kupata namba ya utambulisho wa mlipakodi. Hatua hii itawezesha mama na baba lishe, waendesha bodaboda, bajaji, mafundi seremala na wachomeleaji na wengine wenye shughuli ndogo ndogo kuanzisha biashara zao pasipokuwepo na changamoto ya kudaiwa kodi ndani ya mwaka mmoja. Muda huo tunatoa fursa ya kujiimarisha katika biashara zao wanazozianzisha.

Mheshimiwa Spika, tumetolea mfano huu kwa wafugaji ambao wanajua namna ya kukuza vindama vyao ili baadaye waweze kupata maziwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka nafuu mbalimbali za kikodi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha alizielezea kwa kina zenye malengo ya kuchochea matumizi ya nishati ya umeme na gesi na gesi asilia majumbani na katika sekta ya usafiri kukabiliana na athari zinazotokana na migogoro ya Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Spika, hivyo Serikali itasamehe kodi kwenye vifaa vinavyotumika katika vituo vya ku-*charge* magari yanayotumia umeme na kupunguza ushuru wa forodha kutoka 25% hadi 10%. Nitoe rai kwa wawekezaji wa sekta binafsi kwa ujumla watumie fursa hiyo kuagiza mashine na vipuri vinavyotumika katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta za uzalishaji na katika kutambua kuwa sekta ya kilimo nchini inabeba makundi mengi katika uzalishaji na biashara, Serikali imeweka vivutio mbalimbali vya kikodi ili kuhamasisha kilimo na matumizi ya mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa nchini. Aidha, nafuu hii ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa hii kwa gharama nafuu na kulinda viwanda vya ndani vinavyochakata na kuzalisha mafuta ya kula yanayotokana na michikichi, soya, karanga pamoja na nazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka mazingira bora kwa kuhakikisha kuwa viwanda vya ndani vinazalisha na kuwa na ushindani dhidi ya bidhaa zinazoagizwa nje ya nchi. Hatua hiyo ni sehemu ya kuongeza kiwango cha ushuru wa forodha kwenye bidhaa mbalimbali zinazoagizwa toka nje ya nchi kwa lengo la kulinda viwanda vya ndani na kuhamasisha uwekezaji wa ndani na uzalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, niendelee kutoa rai kwa Watanzania wote kutumia nafuu hizi za kikodi zilizotolewa na Serikali kupitia hotuba nzuri aliyoisoma Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuongeza uwekezaji katika sekta za uzalishaji badala ya kutafuta tu faida binafsi ambazo haziwanufaishi Watanzania walio wengi. Hatua hii itaendelea kutanua wigo wa kutoa ajira kwa vijana ambao kwa sehemu kubwa ndio wamekuwa wenye changamoto nyingi za ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya biashara na uwekezaji nchini, Serikali imefanya maboresho katika sheria 55 ambapo pamoja na mambo mengine ada na tozo 374 zimepunguzwa ama kufutwa. Lengo la hatua hiyo ni kupunguza

gharama za kufanya biashara, kuimarisha mazingira ya uwekezaji pamoja na kuongeza usajili wa biashara na uwekezaji hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni kufanya maboresho katika kanuni mbalimbali kama ambavyo mtakumbuka zilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Hizi ni hatua muhimu ambazo Serikali imechukua kuweka mazingira mazuri ya uzalishaji na wananchi kujiletea maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imezingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kero ya wingi wa ada, tozo na adhabu zinazotolewa na mamlaka za udhibiti wa ufanyaji biashara na uwekezaji. Hivyo Serikali imeridhia kuanzisha mfumo jumuishi ili kutatua kero hizo bila kuathiri majukumu na msingi unaofanywa na taasisi hizo za udhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sekta za kifedha, sekta za kimkakati; Serikali imetoa fedha zaidi katika baadhi ya sekta za kimkakati ili kuwezesha kukamilika kwa miundombinu inayohusika, lengo ni kuimarisha miundombinu hiyo. Mfano upande wa miundombinu ya reli, reli ya kisasa ya *SGR*, ujenzi wa barabara, upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na viwanja vya ndege na bandari zingine pia itajumuisha gharama za usafiri na usafirishaji na kuleta unafuu kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaweka nguvu kubwa vipande vya reli ambavyo havijakamilika Dodoma - Tabora, Tabora - Isaka, Isaka - Mwanza. Ikiwezekana mpaka mwaka 2030 basi tuwe na treni inayotoka Mwanza mpaka Dar es Salaam, Dar es Salaam mpaka Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeboresha kilimo cha umwagiliaji kwa kuongeza ruzuku na pembejeo, uchimbaji wa mabwawa, ujenzi na uboreshaji wa viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa mazao, hatua hii imelenga uzalishaji na thamani ya

mazao kwa wananchi wengi zaidi ambao wanajishughulisha na shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya madini Serikali imetenga fedha za kuweka mazingira wezeshi kwa ujenzi wa viwanda vya kusafisha dhahabu pamoja na madini mengine na uboreshaji wa ramani za kina za madini hapa nchini. Hatua hiyo inavutia uwekezaji na itasaidia wachimbaji wadogo kupata masoko, teknolojia na kuacha kuuza madini yakiwa ghafi yanayopunguza thamani ya madini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa upatikanaji wa nishati ya mafuta, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kisekta ametoka kutoa neno la faraja. Serikali itaendelea kusimamia mpango mkakati ambao sekta Wizara ya Kisekta imeuweka kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ametoka kutuambia hivi punde na yale ambayo aliyafafanua kwa kirefu wakati wa bajeti ya sekta ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wananchi katika majimbo yao wanapata maendeleo kwenye sekta mbalimbali ikiwemo maji, barabara na nishati, kama ambavyo umeona jinsi ambavyo wamefuatilia kwa ukaribu.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo maana halisi kwamba Watanzania walichagua wawakilishi sahihi na wawakilishi hao wanafanya kazi yao kwa usahihi. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa hiyo ambayo mmeidhihirisha kwa vitendo katika kipindi hiki chote mlichokaa kupitisha bajeti za kisekta na Bajeti Kuu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ushauri huo na itaendelea kuboresha utaratibu wa utoaji wa fedha kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge walisemea katika baadhi ya sekta. Kwa mfano, 70% ya fedha za mifuko ya maendeleo zitaelekezwa moja kwa moja kwenye mifuko hiyo. Hapatakuwepo na ucheleweshaji wa

fedha za mifuko ambazo zimeshakusanywa. Kuanzia zinapokusanywa zitapelekwa moja kwa moja kwenye mfuko husika ili mfuko husika uweze kutekeleza majukumu yake ya kimsingi bila kuwa na matatizo ya utoaji wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uamuzi huo utaongeza kasi na uhakika wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kupanua wigo wa huduma za jamii na kuongeza fursa za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwakumbusha watendaji wa taasisi ambazo zitapelekewa fedha hizo kuhakikisha wanakamilisha miradi iliyokusudiwa tena kwa kuzingatia thamani ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka miradi inayojengwa iwe na uimara ili kuepusha fedha za umma kuwa zinapotea kwa kurejea kutengeneza miradi ambayo ilikwishakutengenezwa. Wakumbuke kuwa dhamira na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kutekeleza kikamilifu miradi ya maendeleo kwa ajili ya ustawi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itachukua hatua kali kwa watendaji wote watakaoshindwa kutekeleza maelekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali na Wabunge wote na Watanzania wote naomba nitoe tena shukrani za kipekee kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha za kutekeleza miradi hiyo na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Tumuombee Mungu amjalie afya njema na hekima zaidi na kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais ameonesha kwa vitendo dhana yake ya uwazi na uwajibikaji kwa kuziongezea taasisi zetu za udhibiti, fedha, rasilimali watu na vitendea kazi. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taasisi yetu ya Kupambana na

Kuzuia Rushwa na taasisi zingine zote za udhibiti ili kuweza kuhakikisha kwamba wanafanya kaguzi wakati miradi inaendelea ili pale panapotokea ubadhilifu hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. Hii ni hatua kubwa na ni dhamira ya dhati ya kutunza na kulinda rasilimali za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika ziara nilizofanya maeneo mengi nchini kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi hususani migogoro ya ardhi. Baadhi ya masuala hayo yamekwishafikishwa kwenye Mabaraza yetu ya Ardhi ya Wilaya na baadhi hayakupata fursa ya kufikishwa huko. Baadhi ni kwa ajili ya upungufu wa ikama za Mabaraza ya Ardhi na baadhi ni kwa ajili ya upungufu wa mabaraza yenyewe katika baadhi za wilaya. Mfumo wa Mabaraza ya Ardhi ulianzishwa kwa miaka ya nyuma ikiwa ni wakati Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya zikiwa chache katika maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuangalia upya utaratibu unaotumika kutatua migogoro ya ardhi ili tuweze kupata jawabu la kudumu la kupata ufumbuzi wa migogoro ya ardhi badala ya kutegemea ziara. Tunaangalia uwezekano wa kuangalia namna ya kuboresha ama kuendelea kuboresha mabaraza ama kuhamishia masuala ya ardhi kwenda kwenye mahakama ambazo sasa zipo kila wilaya hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuwa imekamilisha kufanya uamuzi wake, ikitokea kwamba uamuzi utakuwa ni wa kuhamishia mabaraza katika mahakama zetu, Serikali itafanya hivyo kwa uharaka ili Bunge lijalo tuweze kuleta mapendekezo hayo ili tupate ufumbuzi wa kudumu wa namna ya kushughulikia migogoro ya ardhi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Watanzania wote tuache kuendelea kuaminiana aminiana na kupeana ardhi kwa kuaminiana bila kuweka misingi ya kisheria kwa sababu migogoro mingi pia inatokana na kupungua kwa uaminifu baina ya sisi kwa sisi.

Mheshimiwa Spika, pia kwa nyakati mbalimbali nimepokea changamoto wanazokutana nazo baadhi ya wafugaji kwa mifugo yao kutaifishwa baada ya kukamatwa katika maeneo yaliyohifadhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wameongelea sana jambo hili wakiwa hapa Bungeni. Baadhi ya mashauri haya yalikwisha kuhitimishwa katika vyombo vya kisheria kwa wafugaji kupata ushindi na kuamuliwa warejeshewe mifugo yao. Taasisi husika hazijatekeleza maamuzi hayo ya Mahakama na kuishia kuambia mifugo yao ilikufa, ama ilipotea, ama sababu zinginevyo.

Mheshimiwa Spika, vitendo hivyo vinadhoofisha sekta ya mifugo na kuwaacha wananchi hawa katika ufukara. Ili kuimarisha misingi ya utawala bora na utawala wa kisheria na utoaji wa haki kwa wananchi kupitia mkutano ujao wa Bunge, Serikali itawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria zinazosimamia utaifishaji wa mifugo na mali kwenye maeneo yaliyohifadhiwa. Tunakwenda kuifuta sheria hiyo inayotaifisha mifugo ya Watanzania inapokutwa katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa nitumie Bunge lako Tukufu kuwaelekeza Wizara ya Fedha kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii wahakikishe wanatekeleza maamuzi yaliyotolewa na Mahakama, wawarejeshee mifugo yao wafugaji walioshinda kesi Mahakamani na kama mifugo hiyo ilikufa ama ilipotea basi wawarejeshee fidia za mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie hiyo, ninawaelekeza Wizara ya Fedha na Wizara ya Maliasili na Utalii watekeleze maamuzi ya Mahakama yaliyotolewa pale ambapo wafugaji walishinda kesi wawarudishie mifugo yao na kama ilikufa ama ilipotea wawarejeshee fidia ya fedha kwenye mifugo hiyo iliyopotea. Kama nilivyosema ili haya yasijirudie tunakwenda kufuta hiyo Sheria ya Utaifishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatuna maana kwamba hatuzingatii maeneo yaliyohifadhiwa, lakini tunaondoa mianya hii kwa sababu katika baadhi ya maeneo utaifishaji huu umetoa mwanya uliotumika vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambapo mifugo haijafa, imegawanywa na hayo tutaendelea kuyafanyia kazi moja baada ya lingine. Tutachunguza na yenyewe baada ya kuwa tumeshakamilisha haya ya kuwarudishia mifugo wanaohusika na fidia wanaohusika, lakini pia na kufuta sheria hii ambayo imewasababishia vidonda Watanzania wengi wanaoshughulika na sekta hii na tutaendelea kuangalia na sheria zingine ambazo zinahusiana na mambo ya aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengi hapa nchini kumejitokeza vitendo vya baadhi ya watendaji wa mamlaka za udhibiti na usimamizi wa sheria kunyang'anya bidhaa, mitaji na vitendea kazi wajasiriamali na wananchi katika baadhi ya maeneo ya vitengo vyao.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya aina hii havikubaliki na vinarudisha nyuma jitihada za wananchi kujikwamua kiuchumi licha ya Serikali kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha wananchi hao waweze kutekeleza majukumu yao ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nilienda eneo moja nikakuta wanafanya uchunguzi, wamechukua mashine, wamechukua mpaka magodoro. Magodoro na uchunguzi wa jambo la ambalo halihusiani na magodoro yanaingiliana wapi? Hivyo hivyo tumesema vishikilie vitendea kazi tu ambavyo vimeshiriki kwenye makosa ambayo kwa asili ya makosa hayana dhamana. Mauaji, nyara za Serikali, dawa za kulevya, ubakaji na mengine ya asili hiyo.

Mheshimiwa Spika, yale mengine ambayo vitendea kazi vitaweza kuzalisha ili mwananchi aweze kulipa faini, visichukuliwe

vitendea kazi, tubaki tunashughulikia suala la faini ambalo kisheria ndicho ambacho Serikali inatakiwa kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama msimamizi wa shughuli za Serikali nitaendelea kuchukua hatua kali kwa wale wanaopuuza maelekezo haya. Nimewaandikia wakuu wa taasisi zote wazingatie maelekezo haya na wale wanaokiuka kama nilivyosema tumeanza kuchukua hatua kali na tutaendelea kuchukua hatua kali ili kukomesha tabia hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kusisitiza maelekezo haya kwa watendaji wote wa Serikali kuheshimu mitaji ya watu, kuheshimu jasho la Mtanzania, kuheshimu shughuli zinazofanywa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusifanye kuwategeshea tegeshea Watanzania ili tuchukue mali zao, ili tuchukue fedha zao, ili tuchukue faini. Mtu anakwenda kulima na trekta kwenye shamba tunamwangalia, wakati wa mavuno ndio tunaenda kufyeka na kuchoma moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaenda tunafyeka mahindi, halafu pembeni kuna bangi. Lazima maeneo ambayo tumeyahifadhi tuyahifadhi, lakini wakati ule ule tusiendekeze vitendo vya rushwa kwamba yule ambaye hajatoa rushwa tunamfyekea, yule mwingine amelima, yule mwingine tunachukua trekta. Haya hayakubaliki, lazima tuziondoe dosari za aina hii.

Mheshimiwa Spika, haya ni masuala yanayohusu uwajibikaji, nimeongelea yale yanayohusu haki, sasa ninaongelea yanayohusu uwajibikaji. Lazima tutoe kwa wananchi huku tukitekeleza dhana ya uwajibikaji ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza ifanyike kwa ufanisi na ni muhimu sana kwa viongozi na watendaji na watumishi wote kuwa na mahusiano mazuri katika kutekeleza dhana hii ya uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, hali iliyojitokeza katika baadhi ya maeneo kumekuwepo na migogoro na migongano baina ya viongozi, watendaji na watumishi na hivyo kupunguza tija katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Ikumbukwe kuwa ndiyo kwanza tunaenda kuanza utekelezaji wa dira mpya tarehe 01 Julai; ndiyo kwanza tunaenda kuanza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2025 tarehe 01 Julai; ndiyo kwanza tunaenda kuanza kutekeleza bajeti ya kwanza baada ya uchaguzi tarehe 01 Julai. Hivyo basi, ni wajibu wa kila mmoja kujielekeza katika kuwawezesha wananchi kupata manufaa ya mipango hiyo na dira hiyo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi umepita, tumemaliza uchaguzi, sasa twende kufanya kazi. Hali hiyo itawezesha Watanzania kunufaika na mipango mizuri ambayo Mheshimiwa Waziri wa Mipango aliisoma na dira aliyoisoma, na bajeti hii nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametoka kuisoma na Bunge lako Tukufu limetoka kuipitisha. Hali hiyo itawezekana tu kama hatutakuwa na migogoro inayochelewesha utekelezaji wa mipango hiyo na Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, katika usimamizi wa shughuli hizo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, kila mwaka tulikuwa tunaingia gharama za uchaguzi wa viongozi na watendaji wanaingia katika michakato hiyo ya uchaguzi kwenye Serikali zetu za Mitaa. Mazingira haya yalikuwa yanachochea migongano na kuondoa utulivu katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotoka kusema kule, tumemaliza uchaguzi, ndiyo kwanza bajeti ya kwanza tunataka kuanza kutekeleza, ndiyo tarehe moja tunaanza kutekeleza dira na ndiyo tunaanza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Ninapenda kulijulisha Bunge lako Tukufu katika mkutano ujao Serikali itawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria kuhusu nafasi ya Naibu Meya na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. Tutaondoa utaratibu wa kufanya uchaguzi kila mwaka. Lengo likiwa ni kubadilisha mfumo wa sasa ambapo chaguzi hizo hufanyika kila mwaka, na sasa tutaenda

kwenye kuweka uchaguzi ambao uchaguzi ukishafanyika basi uhai wa waliochaguliwa kwenye nafasi hizo za Meya, Naibu Meya pamoja na Naibu Mwenyekiti utakaa katika kipindi chote kama ambavyo inafanyika kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hao, tumemwambia pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali aangalie vipengele vitakavyosaidia kufanya halmashauri zetu zitulie na watu waelekeze akili zao kwenye utendaji kazi na kutatua migogoro, kero za wananchi na kuwatafutia wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa wa mnamaliza uchaguzi wa Naibu Meya, Mwenyekiti wa Halmashauri, wiki inayofuata anaanza kampeni ya uchaguzi unaofuata mwaka ujao, ilani haijaanza kutekelezwa, Meya ama Mkurugenzi wako *busy* kutafuta Mbunge mbadala hata ilani haijaanza kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumemwambia Mwanasheria Mkuu wa Serikali aangalie vipengele ili watu wajikite kufanya kazi. Ninayasema haya kwa sababu katika ziara chache nimekuta katika baadhi ya maeneo, hata Mbunge hajaapa, Mkurugenzi na Meya ama Mwenyekiti wa Halmashauri wako *busy* kutafuta Mbunge mwingine. Naibu Meya hajaanza kazi, Diwani mmoja anatafuta nafasi ya Naibu Meya, ama anatafuta nafasi ya Naibu Mwenyekiti. Haya mambo siyo yanayowafurahisha wananchi. Wananchi wanataka kazi, wanataka miradi ya maendeleo, wanataka maendeleo katika maeneo yao. Mambo ya safu, mambo ya kuwaza madaraka ni mambo ya ubinafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ziara pia nimeshuhudia ziara za viongozi wa kitaifa katika maeneo mbalimbali hapa nchini zimeanza kuwa sasa kama sehemu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo utoaji wa huduma bora. Ziara hizi za viongozi wa kitaifa katika maeneo mbalimbali hapa nchini ni sehemu ya

majukumu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hizo, wananchi wengi wamekuwa wakijitokeza kuwasilisha kero mbalimbali. Baadhi ya kero hizo ilitarajiwa ziwe zimetatuliwa na viongozi waliopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawakumbusha viongozi na watumishi wote wa umma kwamba utatuzi wa kero za wananchi ni sehemu ya majukumu yao ya kila siku. Aidha, ziara za viongozi wa kitaifa ikiwemo ziara ya Waziri Mkuu siyo mbadala wa kutoa huduma hizo kwa wananchi na hivyo niendelee kuwasisitizia Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa, Serikali za Mitaa na mifumo yote iliyopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuanzia ngazi ya kijiji, mitaa, waendelee kutoa huduma hizo ipasavyo bila kusubiri ziara za viongozi wakuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo tetesi katika baadhi ya maeneo, kwamba viongozi wapo kama wamepigwa ganzi. Wanasubiri nini? Wanasubiri *Pdf,* mkeka, teuzi. Haya ni mambo ya ajabu, mambo ya ajabu, kuwa ofisini na kusubiri teuzi ni mambo ya ajabu, haya ni mambo ya ajabu ajabu tu.

Mheshimiwa Spika, niendelee kuwaelekeza; mmepewa dhamana na kwenye barua haujaandikiwa inaisha lini, endelea na kazi na kwa kweli, wale wanaosubiri *Pdf* na wale wanaosubiri mkeka, tutawatoa, lakini wale wanaofanya kazi, wataendelea na kazi kwa sababu tunataka wananchi wapate huduma zilizo bora.

Kwa hiyo, nielekeze taasisi zetu zinazofuatilia mienendo ya viongozi, tubainishieni wale wanaosubiri mkeka, wale wanaosubiri *Pdf*, tuwatoe ili tuwaweke watu wanaotaka kufanya kazi. Hatutaki shughuli za ofisi za umma zisimame kwa sababu kuna watu wanasubiri uteuzi. Haya ni mambo ya ajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunajua kuna kifo, hivi tungekuwa tunasubiri kufa kuna mtu angefanya kazi? Unasubirije uteuzi na una jukumu umepewa la kufanya? Ninalisisitiza tena, suala la teuzi, tena teuzi zinazofanyika kwa *pleasure* ya anayeteua, zisisubiriwe, msisubiri tuendelee na kazi. Watu waendelee na kazi! Tunataka watu wakimbie mchakamchaka kuhudumia Watanzania na wale ambao hawatasikiliza maelekezo haya, kwa kweli watakuwa wameshajitambulisha kuwa wamechoka, hawastahili kuendelea kuwa ofisini.

Mheshimiwa Spika, viongozi na watendaji katika kila ngazi, wasimamie na kutekeleza kikamilifu maagizo na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na viongozi wa kitaifa, ikiwemo kutatua kero za wananchi, ikiwemo kuwasikiliza wananchi, ikiwemo kusimamia miradi ya maendeleo. Haya ni majukumu ya kila siku na watenge siku za kusikiliza, watenge siku za kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Taasisi zote zinazotoa huduma, watenge muda wa kutatua kero wananchi wanazozipata kupitia huduma wanazozitoa.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kwa wananchi wote, kuwa pamoja na Serikali na pamoja na uwepo wa ziara za viongozi wakuu wa kitaifa, waendelee kuthamini mfumo wetu wa kiutawala ndani ya nchi yetu. Tumesogeza huduma kwa kila mwananchi. Watumie fursa hiyo kufika katika ofisi za umma ili waweze kutatuliwa yale ambayo yanahitaji ufumbuzi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, ninalisisitiza, ziara zinazofanywa na viongozi wakuu ikiwemo ziara ya Waziri Mkuu, si mbadala wa mifumo rasmi ya utendaji wa kazi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kutumia ziara kama sehemu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa maelekezo, sehemu ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, sehemu ya kuchochea shughuli za maendeleo, na sehemu ya kutatua kero za wananchi. Nina uhakika Wakuu wa Idara, Wizara, Idara, Mikoa, Wilaya na wataalamu katika

maeneo mbalimbali ya Serikali wanao uwezo wa kutatua changamoto hizo. Mheshimiwa Rais amewapa dhamana ya kumwakilisha katika maeneo hayo mlipo, kila mmoja atimize wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, sambamba na mifumo hii ya kiutawala, Serikali pia imeweka mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya wananchi kuwasilisha kero na maoni mbalimbali Serikalini. Mifumo hiyo ni pamoja na *e-Mrejesho, e-Kiongozi,* Sema na Waziri, pamoja na Kituo cha Kitaifa cha Mawasiliano ya Simu yaani *call centre* na Waheshimiwa Mawaziri niwapongeze sana mmeanza kulitekeleza hilo kwa kasi na wananchi wameanza kunufaika nalo. Nitoe rai kwa wananchi kutumia fursa hizo ili kuweza kuhakikisha kwamba tunapata ufumbuzi wa yale ambayo tunataka yapate ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Kituo cha Mawasiliano cha Simu kimeongeza wigo wa wananchi kufikisha malalamiko yao bila gharama. Kwa hiyo, kituo hicho pia kiendelee kutumika ili kuweza kuhakikisha wananchi wanapata tija na kupunguza gharama.

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Bunge wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu, ulikuwa mahususi kwa ajili ya kujadili na kupitisha bajeti na mpango wa Serikali. Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2026/2027 ni nyenzo ya kwanza katika kutekeleza Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Mitano yaani 2026/2027 hadi 2030/2031 ambao unatafsiri kwa vitendo Dira ya 2050.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyopitishwa na Bunge lako inalenga kuimarisha miundombinu, kuongeza uzalishaji, kuboresha huduma za kijamii, kuimarisha uwekezaji ndani ya uchumi ili tuweze kufikia uchumi shindani na ustawi wa wananchi. Ili kufanikisha haya, tutaendelea kuimarisha yale ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliyatoa kama maelekezo mahsusi ya kuweza kufanikisha utekelezaji wa bajeti hii ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na maandalizi muhimu ya kuwapokea wanafunzi zaidi ya milioni tatu wa makundi rika mawili yanayotarajiwa kujiunga na elimu ya sekondari ifikapo mwaka 2028. Takribani kata 315 zimebainika kuwa na changamoto ya msongamano wa wanafunzi. Haya yote, Serikali itayazingatia kama sehemu ya kipaumbele kuweza kutatua. Shilingi trilioni 1.7 zitahitajika kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kabla ya Januari, 2028. Hivyo, ninatoa wito kwa wadau wote wa elimu, kushiriki kikamilifu katika kufanikisha maandalizi ya mapokezi ya wanafunzi makundi rika mawili mwaka 2028.

Mheshimiwa Spika, hili ni badiliko kubwa kufanyika ambalo linafuatia baada ya lile ambalo Mwalimu Nyerere alilifanya akiwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lile ambalo lilihusisha kutoka kwenye elimu ya lazima ya darasa la nne kwenda lile la saba. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anapeleka hatua nyingine ya kihistoria ya elimu ya lazima ya miaka 10. Kila mmoja wetu anayo nafasi ya kuchangia katika mabadiliko haya na kufikia azma ya kupata miundombinu muhimu na kuwawezesha wanafunzi tarajiwa wote kuanza masomo kwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, nikiwa naelekea kumalizia nisisitize jambo moja muhimu nalo ni suala la usalama, amani na utulivu. Uwepo wa amani umeendelea kuwa msingi muhimu wa shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Haya yote tuliyoyapanga kwenye dira, haya yote tuliyoyapanga kwenye mipango ya maendeleo ya miaka mitano na ile ya mwaka mmoja mmoja, yale yote tuliyoyapanga kwenye ilani ya uchaguzi na yale yote ambayo tumeyapitisha kwenye bajeti itakayoanza Julai Mosi, hayawezi kuwa na manufaa kwa Watanzania, wala hayawezi kutekelezeka pasipo amani, usalama na utulivu ndani ya nchi yetu. Hivyo basi, uwepo wa amani umeendelea kuwa msingi muhimu wa shughuli zote za kiuchumi, kijamii na kisiasa na hivyo kuifanya nchi yetu kuendelea kuvutia uwekezaji na kuimarisha ustawi wa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania tunao wajibu wa kutunza hali hii bila kujali tofauti zetu za kidini, kisiasa au kikabila. Nitoe rai kwa kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa analinda na kuitunza tunu hii ya amani na utulivu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninawasisitizia Watanzania wenzangu wote tuendelee kulinda amani tuliyoirithi kutoka kwa waasisi wa Taifa letu huku tukizingatia sheria, kuheshimu haki za wengine, kujiepusha na vitendo vinavyoweza kusababisha migawanyiko ndani ya nchi yetu. Tuzingatie matumizi ya lugha za staha katika mijadala ya kijamii na kisiasa, kwani nayo yana mchango mkubwa wa kuvunja mshikamano ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, amani ikivunjika, utulivu ukitoweka, umoja wetu ukivunjika, hakuna anayebaki salama. Hivyo, wale wanaojihakikishia kubaki salama hasa hasa wale wasiyo Watanzania ama wale walio nje ya Tanzania, wasituongoze katika kuvunja amani yetu, utaifa wetu na Taifa letu. Amani, utulivu na mshikamano wa Taifa hili si vitu vya kuchezewa, kwani vimejengwa kwa jasho, uzalendo, damu na hekima ya waasisi wa Taifa letu. Kwa namna yoyote na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Mambo ya Ndani ametoka kutoa kauli na mwongozo ambao Serikali itausimamia. Kwa namna yoyote, Serikali haitaruhusu amani, utulivu na utaifa wetu uharibiwe na yeyote yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote ni mambo ambayo wala tusidanganyane, wala hatutaruhusu yachezewe, wala tusidanganyane suala la usalama, amani na umoja wa nchi yetu, wala si mambo ya kujadiliwa, wala tusidanganyane. Wala hatutaruhusu yaharibiwe na wale wanaoelekeza kwa ma-*group* ya *WhatsApp*, waje wenyewe. Wasitumie Watanzania kama chambo. Wana mambo yanawasukuma, waje wenyewe, wasielekeze kwa ma-*group* ya *WhatsApp*, wasikae huko na kutumia simu na mitandao na ma-*group* ya *WhatsApp* kuchochea vurugu kwenye nchi yetu, waje wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasiwatume watoto wa Kitanzania, wasifanyie biashara maisha ya watoto wa Kitanzania, kuwatuma kwa ma-*group* ya *WhatsApp* kwamba tukutane pale, tukutane pale, tukutane pale, wao wakiwa kwenye mataifa mengine kule, wakiwa wanahifadhiwa kwenye mataifa mengine, wanatunzwa, wanalishwa, halafu watumie ma-*group* ya *WhatsApp* kuwatuma watoto wa Kitanzania, waje wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nchi hatutaruhusu nchi yetu ichezewe, wala hatutaruhusu amani ya nchi yetu ichezewe na mtu yeyote yule. Tutalinda nchi yetu, tutawalinda Watanzania, tutawalinda watoto wa Kitanzania dhidi ya wale wanaotaka kutumia biashara maisha ya watoto wa Kitanzania. Tanzania ni nchi yetu sote na hatutakuwa tayari kuona mtu yeyote ama kikundi chochote chenye masilahi yoyote kulitumbukiza Taifa letu katika migawanyiko, vurugu, machafuko na kusababisha matatizo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, umoja wa Watanzania siyo jambo la mjadala, ni msingi wa uwepo wa Taifa letu na ni wajibu wa kila mmoja kuutunza. Hivyo, Watanzania wote ambao tumeipenda nchi yetu nzuri tuliyopewa na Mungu kwa miaka yote hii tusiingie kwenye mtego wa wale wenye tamaa na wenye masilahi yao binafsi na hasa hasa wanaotolea macho rasilimali za Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hili ni Taifa moja, Taifa lililojengwa kwenye misingi ya kindugu, Taifa lililojaaliwa rasilimali nyingi wala hatutagawanyika wala hatutaingia kwenye mtego huo. Tulishavuka mitego hiyo siku nyingi. Tumevuka mitego ya udini, mitego ya ukabila, mitego ya vyama vya kisiasa, mitego ya ukanda, na sasa tunalo Taifa moja lililojengwa katika misingi ya utawala bora na demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, suala la usalama, amani na utulivu ni kipaumbele namba moja na hakuna mjadala katika hilo. Niwahakikishie Watanzania na niwahakikishie Waheshimiwa

Wabunge, Serikali iko imara, tena imara sana kwenye jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwasihi Watanzania wote kuheshimu misingi ya utawala bora na kuhakikisha kwamba shughuli mbalimbali za kijamii, kiutamaduni, kidemokrasia na kiuchumi zinazingatia sheria, taratibu, mila, desturi na Katiba yetu ya nchi. Tunayo Katiba ya nchi yetu ndio inayotuongoza, hakuna sehemu Katiba yetu imesema sasa tutakuwa tunapeana matamko tu, siku fulani tunataka tufanye fujo, Katiba haijasema hivyo.

Mheshimiwa Spika, hakuna sehemu ilipoandikwa kwenye Katiba kwamba tutakuwa tunafanya siku fulani tunakaa tu tunapanga, hatuna kazi nyingine, tunakaa tu tunapanga tu tunatangaza kwamba siku hiyo tutakuwa tunafanya hivi. Hatuwezi tukaendesha nchi kwa namna hiyo. Hatuwezi tukaendesha nchi kwa taratibu hizo kwamba watu wanakaa tu sijui Taifa gani huko wanakaa tu huko wamejifungia wanalishwa, wanalipwa, wanatutajia tarehe tu kwamba tarehe hii tutakuwa na jambo hilo. Hatuwezi tukaendesha nchi kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ambaye nimeshazisoma sana historia za mataifa yenye rasilimali nyingi hapa Afrika ninaijua hiyo michezo yote na ninafuatilia kuna baadhi ya ofisi zinatajwa kwenye hivyo vipeperushi vinavyotajwa tajwa hivyo. Tutaendelea kufuatilia na kila nikifuatilia wakitajwa sijaona wakikanusha kwamba mkifanya hapa, mkifanya hapa, mfanye na hapa muende na hapa, mfanye na hapa, ninaziona.

Mheshimiwa Spika, sasa wengine tulizaliwa bila uoga, tutafuatilia moja baada ya nyingine, lakini uhakika mmoja ninaowaambia tunafuatilia yote hayo, tunafuatilia yote hayo. Tunawaambia kama hao wanaoandika andika ma-*group* ya *WhatsApp* hayo wakiwa huko, tunawaambia wao na wanaowatuma, hatuwezi kutetereka kwenye jambo la kuilinda nchi yetu na rasilimali zake. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Rudia hapo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, anasema, rudia hapo.

Mheshimiwa Spika, tunawaambia wanaowatuma na wanaotumwa, hatuwezi kutetereka kwenye kuilinda nchi yetu na rasilimali zake na watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutailinda nchi yetu, tutawalinda Watanzania, tutalinda rasilimali zake na wala hatutaruhusu watoto wa Kitanzania watumike kibiashara na wale wenye masilahi yao binafsi. Suala la amani ya nchi yetu siyo jambo la mjadala na suala la usalama wa nchi yetu siyo jambo la mjadala.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Sekta, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi amelielezea kwa kirefu. Ninasisitiza yale ambayo Mheshimiwa Waziri ameelekeza, taasisi zote zisimamie na zifuatilie kila hatua, wananchi endeleeni na shughuli zenu za kila siku, nchi iko salama na wala hatutaruhusu michezo michezo iwatoe wananchi kwenye kutekeleza shughuli zao za kimaendeleo. Hatutaruhusu michezo michezo hii iwatoe Watanzania kwenye shughuli zao za kila siku za kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ni ya kibiashara tu, mambo mengine wanaona nchi inapiga hatua, wanaona nchi imefanya ugunduzi wa rasilimali nyingi, wanaanza kuleta chokochoko hizo. Mungu alitugawia kila mtu na nchi yake, kila watu walipewa nchi yao. Tanzania ni nchi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi niendelee kumalizia; kutokana na umuhimu wa sekta ya michezo, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali na kuchukua hatua mahsusi za kuinua sekta hii muhimu kwa uchumi wa Taifa letu. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo, kuanzisha Tuzo za Michezo za Baraza la Michezo la Taifa kwa lugha nyingine *The National Sports Council*

*Sports Award,* kuwezesha timu za Taifa kushiriki mashindano mbalimbali na kuimarisha miundombinu ya michezo na kutenga fedha kupitia bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuratibu mashindano ya UMISETA na UMITASHUMTA kwa lengo la kuinua vipawa vya watoto na kuendelea kuvilea. Hatua hiyo imetekelezwa sambamba na kuwekeza kwenye akademia za michezo, kuwezesha makundi maalumu kushiriki katika mashindano mbalimbali pamoja na kuhamasisha mashindano kuanzia ngazi za chini na kuwezesha mashindano katika timu za chini ya miaka 18.

Mheshimiwa Spika, licha ya kutoa burudani, sekta ya michezo pia imekuwa ni sekta inayotoa ajira. Kwa upande mwingine mafanikio haya katika sekta ya michezo yamechochewa na utashi mkubwa wa kisiasa na utashi mkubwa wa kuendeleza michezo kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ametoa mwelekeo na kwa wakati wote ameweza kuweka chachu na tumeona mafanikio ya timu ya Taifa, lakini pia na timu za Taifa pamoja na vilabu vya hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi tena kwa mara nyingine kwa timu ya wanawake chini ya miaka 20 - *The Tanzanite Queens,* kwa kufuzu kihistoria kushiriki Kombe la Dunia la *FIFA* la Wanawake litakalofanyika nchini Poland kuanzia tarehe 5 hadi 27 Septemba, 2026. Vilevile, timu ya Taifa ya mpira wa miguu ya wanawake - *Twiga Stars,* waliofuzu Kombe la Mataifa ya Afrika la Wanawake 2026 ambayo itafanyika kuanzia mwezi Julai, 2026 kule Morocco. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninawapongeza vijana wetu, timu ya vijana chini ya umri wa miaka 17 - *Serengeti Boys,* kwa kufanikiwa kufuzu Fainali za Kombe la Dunia la *FIFA* 2026 zitakayofanyika nchini Qatar kuanzia tarehe 19 Novemba hadi 13 Disemba, 2026. Timu hiyo pia ilimaliza mshindi wa pili katika Fainali za Kombe la Mataifa Afrika ya vijana chini ya miaka 17 iliyomalizika kule nchini Morocco 2026.

Mheshimiwa Spika, hatukuzoeazoea timu za Taifa za Tanzania zinacheza Kombe la Dunia, tunasikia tu fainali kombe la dunia, kombe la dunia, kombe la *AFCON,* kama ambavyo tumeona sasa hivi timu zote. Huu ni mwanzo mzuri, tunakoelekea ipo siku tutakuja na vikombe hapa. Juzi vijana wa miaka 17 wamekikosa kosa kikombe, mwaka juzi Simba wamekosa kosa kombe, mwaka juzi kabla ya hapo Yanga wamekosa kosa kombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sisi wafugaji tulikuwa tunasema kama unaona wingu kubwa mvua hainyeshi, kuna siku hata bila wingu kubwa itashuka mvua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hii ya timu zetu za Taifa na vilabu vyetu hivi inatupa ishara kwamba kikombe kiko karibu cha Afrika ama cha dunia kitatua hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo kwa upande wa ngumi, nitoe pongezi kwa mabondia wetu, bondia Ibrahim Class, ambaye amefanikiwa kutoa mikanda miwili mikubwa *WBC*. Mikanda hiyo imeweka historia kubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na ushindi huo michezo ya klabu pia kwenye upande wa kikapu *Dar City* ilifuzu na kushiriki mashindano ya *Basketball African League* ambayo kama nilivyosema ni hatua nyingine pia kubwa ambazo zinaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa ninaelekea kumalizia nitoe shukrani zangu za dhati tena kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake bora ambao ameuonesha na mapenzi yake kwa Watanzania ambapo umeona ambavyo amekuwa akisimamia rasilimali, lakini pia na miongozo yake katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi nyingine kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kazi kubwa anayofanya ya kumsaidia

Mheshimiwa Rais katika majukumu hayo kama msaidizi wa Rais; na tatu kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kazi kubwa anayofanya ya kuwaletea Wazanzibari maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee pia nikushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kazi nzuri unazofanya, umeonesha usimamizi bora wa Bunge lako Tukufu. Bunge linalotanguliza masilahi ya Watanzania mbele, Bunge la Watanzania. Nikupongeze sana, na ninawapongeza wasaidizi wako; Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, pamoja na Wenyeviti wote wa Kamati ambao wanakusaidia katika shughuli hizi za kuliendesha Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Profesa Palamagamba Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge wa Kilosa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge, Uratibu na Wenye Ulemabu, pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wote walioko Ofisi ya Waziri Mkuu na Mawaziri wote na Naibu Mawaziri wote wanaounda Baraza la Mawaziri kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimpongeze pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali Ndugu yangu Hamza Johari kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya. Mmeudhihirishia umma wa Watanzania kwamba ninyi linapofika jambo la masilahi ya nchi yetu hamna urafiki na hamna mzaha, na tumeona katika hoja zilizokuwa zinajitokeza tangu tulipoanza Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hongereni sana kwa kazi nzuri mliyofanya hapa. Rai yangu kwenu tutakapomaliza Bunge basi muende majimboni ili mkawafafanulie waheshimiwa wananchi wa Tanzania katika majimbo yenu yale masuala mliyoyapitisha katika bajeti yetu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka - Katibu Mkuu Kiongozi, kwa ushirikiano wake wakati wa utekelezaji wa majukumu haya. Amekuwa kiungo muhimu na amekuwa msaada sana katika kuendesha haya majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe pia pongezi kwa Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Jaji Mkuu wa Tanzania, kwa misingi ya uwajibikaji kuwa ni mhimili mwingine ambao unatusaidia kama nchi kuweza kutekeleza majukumu haya ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nivipongeze vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vyote kwa ujumla wao vikiongozwa na Mkuu wa Majeshi, *CDF* Jenerali Mkunda, pamoja na timu yote ya vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa ninamalizia, kipekee kabisa niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Iramba, wananchi wangu ambao wamekuwa nami wakitambua majukumu makubwa ambayo ninayatekeleza, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia familia. Nikianza na mke wangu mpenzi, Bi. Neema Mwigulu Nchemba, pamoja na watoto Joshua, Gracious, Isack, Benice, kwa umoja wao na mshikamano ambao wameendelea kuniombea nikiwa ninatekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nikipongeze chama changu, Chama Cha Mapinduzi, ambacho bajeti hii imezingatia ilani yake, chini ya Uenyeekiti wa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Katibu Mkuu,

Dkt. Asha-Rose Migiro, kwa kazi kubwa ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona katika maeneo yetu jinsi ambavyo ufuatiliaji wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ambao umekuwa ukifuatiliwa.

Mheshimiwa Spika, nikamilishe salamu zangu kwa kuwapongeza na kuwashukuru wenzetu wa sekta binafsi ambao wamekuwa wabia muhimu katika shughuli za maendeleo, sekta binafsi, viongozi wa dini pamoja na taasisi zisizo za kiserikali ambao wamekuwa wakishirikiana nasi. Endeleeni kufanya kazi yenu kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa. Ninyi ni nguzo muhimu ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru pia wenzetu wote ambao wamewezesha mkutano huu; waandishi wa habari, madereva na wote ambao wametusaidia wakati tukiwa katika shughuli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, ninaomba sasa Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tutakapokutana tena tarehe 25 Agosti, 2026, saa 3.00 asubuhi hapa Ukumbi wa Bunge, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, na leo hoja imeungwa mkono mpaka na Ado na timu yote ya upinzani. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji hoja ya kuahirisha Bunge mpaka 25 Agosti, 2026 saa 3.00 asubuhi.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI**

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Naona Mheshimiwa Ado leo suti uliyovaa hiyo. Mheshimiwa Ado hiyo suti uliyovaa leo, imekupendeza sana. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri yenye matumaini makubwa ya kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dkt. James Kilabuko - Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, mgeni wa Mheshimiwa Patali Shida Patali, Ndugu Alfayo Kanandi, Mwinjilisti kutoka Mkoani Mbeya, *(Makofi)*

Wageni 130 wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, wananchama wa *FEMA Club* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wawakilishi 14 wa taasisi ya *JJ Group* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Wabunge; mnatangaziwa kuwa Ofisi ya Bunge imeandaa Jarida la Bunge, Toleo la 12. Jarida hili linaeleza masuala mbalimbali ya Kibunge ikiwemo matukio yaliyojiri wakati wa Mkutano wa Tatu wa Bunge. Jarida hilo limeshawekwa kwenye vishikwambi vyenu na mengine mtagawiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, Mwenyekiti na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, mlezi wa kundi la Wabunge Waislamu ndani ya Bunge wanaomba kutoa shukrani zao za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote na watumishi kutoka imani tofauti waliochangia kwa ukarimu katika kufanikisha programu ya mfungo wa mwezi wa Ramadhani. *(Makofi)*

Kupitia michango yao ya kifedha tulifanikiwa kukusanya shilingi milioni 12 na kutuwezesha kusaidia taasisi 10 ambazo ni Shule ya Sekondari ya Bunge, Shule ya Sekondari ya Dodoma, Gereza la Isanga, Gereza la Msalato, Msikiti wa Nzuguni, Kituo cha Yatima cha Swabrina - *Area D*, Madrasa Rahim - Mkungi, Madrasa Maruah - Chinangali, Madrasa Fatiha *Ipagala North* na Madrasa ya Kijiji cha Mkoka. *(Makofi)*

Ukarimu wenu umeonyesha moyo wa upendo, umoja, huruma na mshikamano wa Tanzania. Haya ndiyo maisha ya Watanzania. Tunaishi kwa *co-existence*. Tunaishi kwa pamoja bila kubaguana kwenye dini, kabila wala rangi. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge na kuwakumbusha kuwa *JJ Group Companies Limited* yenye makao makuu yake eneo la Ilazo, Jijini Dodoma wameandaa Tamasha la Usiku wa Urithi wa Taifa lenye lengo la kuhifadhi, kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu fasihi asilia pamoja na urithi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Tamasha hilo linalenga kuwakutanisha wadau mbalimbali wa utamaduni, viongozi wa Serikali, viongozi wa kisiasa,

wafanyabiashara na wananchi kutoka makundi mbalimbali ya kijamii ili kujifunza, kubadilishana uzoefu na kuendeleza utamaduni wa Watanzania.

Tamasha hilo litafanyika leo siku ya Ijumaa tarehe 26 Juni, 2026 kuanzia saa 1.00 jioni hadi saa 6.00 usiku katika ukumbi wa *Midland Hotel,* Dodoma. Mgeni rasmi wa tamasha hili atakuwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wabunge wote wenye nafasi mnaombwa kuhudhuria. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia kuwa Kikundi cha Kijana Ajira kinajichojihusisha na miradi ya *Asali Wild screen Festival* kimeandaa *NB Asali festival 2026 Utalii Plus* kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo ndani ya Mkoa wa Tabora sambamba na asali ya Tabora kwa kufanya matembezi kuzienzi hatua walizotembezwa babu zetu zama za utumwa. Matembezi haya yataanza *Tabora Zoo* kwa ajili ya utalii wa wanyamapori kisha safari kuelekea tembe la Dkt. Livingstone Kwihala mahali palipowekwa kambi kwa ajili ya *festival*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tamasha hili linatarajiwa kufanyika kwa siku tatu kuanzia tarehe 13 mpaka 15 Agosti, 2026 kwa ajili ya wajasiriamali kuuza bidhaa sambamba na mnyororo wa thamani wa mazao ya nyuki na asali ya Tabora. Ada ya kushiriki ni shilingi 50,000 kwenda mpaka shilingi 100,000. *VIP* ni Dola za Kimarekani 100, watalii kutoka nje ya Tanzania watakuwa Dola za Kimarekani 100 na wamiliki wa magari ya kifahari watakaopenda kushiriki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kushiriki tamasha hili na kwa maelezo zaidi wasiliana na Ndugu Shomari Ibrahim kwa namba ya simu 0652130898. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Waziri Mkuu tarehe 01 Julai tunaanza utekelezaji wa *Visiyon 2050*. Bila amani hatuwezi kufika mbele, lakini bila ya watendaji wa Serikali, wanasiasa,

Wabunge, kufanya kazi pamoja kumsaidia Rais kutimiza azma yake ya kuwasaidia Watanzania, hatutaweza kufanikiwa. Lazima tushirikiane kwa pamoja kuunga mkono jitihada za Serikali ili Taifa letu liweze kuwa katika kiwango cha juu cha uchumi. Nina jedwali hapa la miradi ya mkopo wa Serikali wa dola za Kimarekani bilioni 2.5 kutoka Serikali ya Korea. *(Makofi)*

Kuna baadhi ya maeneo bado Serikali hamjakamilisha upembuzi yakinifu. Pesa zipo, tumezikalia na wala hatuhangaiki nazo.

Nampongeza Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri wa Afya, wamehangaika pamoja na watendaji wa Wizara yao na kuheshimu azma ya Mheshimiwa Rais ya kuleta pesa hizi Tanzania na mkopo huu unalipwa kwa kipindi cha miaka 40. *(Makofi)*

Ni mahusiano ya Tanzania, Mheshimiwa Rais yaliyofanya Korea watoe mkopo huu kwa miaka 40. Sasa pesa zimeletwa na Rais watendaji wa Serikali wote tumekaa kimya kutokushughulikia utaratibu wa kuzipata hizi pesa. Nitazisoma taasisi. *(Makofi)*

Hospitali ya Muhimbili washapata milioni 363, hongera sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wako; uanzishaji wa chuo cha teknolojia cha kidijitali *USD* milioni 167; Wizara ya Fedha imewasilisha maombi ya fedha kwa Serikali ya Korea, hongereni sana. Serikali ya Korea imepokea maombi ya mkopo, lakini bado hawajaidhinisha mkopo, inatakiwa kufuatilia. *(Makofi)*

Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Bagamoyo milioni 202; Tume ya Mipango imetoa maoni kuhusu taarifa ya upembuzi yakinifu Desemba 2025, Serikali ya Korea haijapokea maombi ya mkopo. *Feasibility study* imekwenda, maombi ya mkopo hayajakwenda. *(Makofi)*

Awamu ya kwanza ujenzi wa kongani ya viwanda Bagamoyo milioni 109, Wizara ya Fedha imewasilisha maombi ya upembuzi

yakinifu Novemba, 2024; Serikali ya Korea haijaidhinisha msaada wa upembuzi huo lakini mpaka Juni, 2026 baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu Wizara ya Fedha itawasilisha maombi ya mkopo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha uko wapi?

Ujenzi wa *studio* ya filamu dola milioni 165, Wizara ya Fedha itawasilisha maombi ya ya *feasibility study*, iliwasilisha Novemba, 2024. Kwa hiyo, vitu hivi Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa watendaji, vinataka vifuatiliwe. Kama havikufuatiliwa mtamsumbua Mheshimiwa Rais, mtamsumbua Waziri Mkuu, mtawasumbua wananchi kutokupata maendeleo wanayotaka kuyapata. *(Makofi)*

Ujenzi wa barabara kilometa 246 Zanzibar, *USD* 298; Wizara ya Fedha inasubiri Mkutano wa *Policy Dialogue*. Harakisheni haya mazungumzo. Mimi nilikutana na Balozi wa Korea juzi, yeye na mimi pamoja na Waziri wa Mipango Profesa Kitila Mkumbo na wako tayari hata kama kuna *priority* zingine za miradi hii ambayo mnaona ina *quick wins* wako tayari kuibadilisha. Kama mahitaji ya Bandari ya Bagamoyo, Bandari ya Dar es Salaam, kuna milioni 429 uwekezaji wa nini... *(Makofi)*

Kwa hiyo mimi nafikiri Serikali hebu jaribuni kupitia *priority* zenu, tazameni *priority* zitakazogusa masilahi ya wananchi wa Tanzania. Uongezaji wa thamani wa madini, *USD* milioni 475, hizi zinaweza zikatumika hata kwenye *refinery*. Mheshimiwa *AG* uko hapa, mnaweza mka-*switch* hii miradi mkaipeleka kwenye miradi ambayo ukiweka tu pesa inaingia. *(Makofi)*

Uwezeshaji wa Shule ya Usafiri wa Anga *USD* milioni 81. Wizara ya Fedha inasubiri Mkutano wa *Policy Dialogue*. Msisubiri, mwenye kuhitaji ndiyo anayekwenda kuhakikisha miradi hii inatekelezwa. *(Makofi)*

Ujenzi wa Bandari Wete, milioni 176, Wizara ya Fedha inasubiri mkutano. Ujenzi wa Barabara ya Mahenge – Ifakara dola za Kimarekani 154, Wizara ya Fedha inasubiri mkutano. Kamati ya Bajeti

mko mnasikia hapa, jedwali hili mnalo, nataka tunaporudi Agosti hapa mnipe taarifa na ninyi mmefuatilia wapi mikutano hii ifanyike na pesa hizi zije, wananchi wa Tanzania waone raha ya nchi yao. *(Makofi)*

Ujenzi wa barabara ya Mahenge tayari ipo miradi kadhaa ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi *(PPP)* ambayo utekelezaji wake haujaanza licha ya umuhimu wa miradi hii katika kukuzwa uchumi wa Taifa. *(Makofi)*

Hii ni pamoja miradi ambayo ipo kwenye *pipeline; Commuter Rail Metro Dodoma*, Reli ya Mtwara – *Mbamba Bay* pamoja na tawi la Songea – Ludewa, Reli ya Tanga – Arusha – Musoma kilometa 1,000, mradi wa kufua kusambaza umeme wa maji Rumakali megawati 222, Mradi wa Bwawa la Kikonge, ufuaji wa usambazaji wa umeme wa umwagiliaji megawati 322, mradi wa umeme wa jua Manyoni megawati 100. *(Makofi)*

Mradi wa umeme jua wa Manyoni mwingine megawati 75, uendelezaji wa Bandari ya Bagamoyo eneo la Mbegani *(TPA)*, Mradi wa maji kutoka Mto Ruvu kuja Dar es Salaam. (Makofi)

*Kibaha – Chalinze Expressway*, hapa nampongeza Waziri wa Ujenzi, Ndugu Ulega, wameshatoa tangazo la kimataifa, nimeliona mwenyewe la kutangaza miradi ya barabara hii. Tunataka watu, kuna neno la kizungu linaitwa *grit, consistency*, *commitment*, *dedication*. Uongozi siyo vyeo, uongozi ni namna gani mtawanyanyua Watanzania kutoka hali ilivyo na kwenda mbele. *(Makofi)*

Fuateni nyayo za Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatafuta pesa, anahangaikia watu ili wananchi wake wafaidi. Sisi wote tumekaa *business as usual*. Niwaombe sana kuanzia mwezi Agosti tutaanza kushikana mashati humu ndani. *(Makofi)*

*Kibaha - Chalinze Expressway* kilometa 78, Mheshimiwa Ulega ameshatangaza, hongera sana Mheshimiwa Waziri. *Chalinze – Morogoro Express* sehemu ya mradi kilometa 205. *Igawa – Tunduma Road* kilometa 218. *(Makofi)*

*In and Outer Rings Road Dar es Salaam*, *Commuter Rail Dar es Salaam*, Dar es Salaam imeemelewa sasa hivi. Kukiwa na *metro* Dar es Salaam katikati mtaona wananchi wanavyochangamkia biashara zao. *(Makofi)*

Nasema tena, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuanza kutekeleza baadhi ya miradi ya *PPP* hususan Wizara ya Ujenzi chini ya usimamizi wa Waziri Mheshimiwa Ulega na watendaji wake kwa kuonesha nia ya dhati ya kuanza utekelezaji wa miradi ya *PPP* katika mwaka wa fedha 2026/2027 ambapo barabara sita ambazo nishazitaja zitatengenezwa. *(Makofi)*

Ni rai yangu kuwa Serikali iweke kipaumbele kwenye miradi yenye tija ambayo itailetea nchi yetu maendeleo kwa haraka, itakayotuletea pesa mapema baada ya utekelezaji wake. Aidha, nasisitiza Kituo cha *PPF Center* kiimarishwe, kuwe na *One Stop Center* halisi kwa kupunguza hatua za mamlaka nyingi za uendeshaji. *(Makofi)*

Wawekezaji wengi wanalalamika, kuna mwekezaji yuko hapa nchini miaka mitano, nenda huku rudi huku. Kuwe na *center* moja tu, akishindwa tunamleta hapa tunamwajibisha. Sasa hatujui nani anayekwamisha miradi sababu wapo ni wengi. Kuna *clusters* za maeneo mwekezaji inabidi aende, tuache mambo hayo. *(Makofi)*

Kuna nchi ya jirani hapa ndogo tu, ni *One Stop Center* kweli kweli. Mheshimiwa Waziri Mkuu, 2030 wananchi wanataka kuona mambo haya yamenini. Bajeti ya *PPP* ni ndogo sana Waziri wa Fedha. Miradi hii ili Tanzania ifanye *feasibility study* inahitaji pesa. *(Makofi)*

Tuwekeze kwenye miradi ya *feasibility study* ili watu wa *PPP* waweze kufanya kazi zao. Tukitegemea *feasibility study* kutoka nje ndiyo maana Tanzania tunapoteza mapato. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakuomba sana, bila *PPP* kuwezeshwa hawawezi kufanya kazi hii. Bunge sasa halitaki mikakati, linataka *results*, tunataka *results*, wananchi wanataka matokeo. *(Makofi)*

Baada ya maneno haya niwaombe safari njema kurudi majimboni, niwatakie kila la kheri. Mungu awajalie mwende salama, mrudi salama tuweze kushirikiana na Serikali kujenga Taifa letu.

Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka tarehe 25 Agosti, 2026. *(Makofi)*

*(Saa 6.57 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 25 Agosti, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*